

NI MIMI

 Nimeitwa mpindukia mipaka, kwa hiyo nadhani ndivyo nilivyo katika kusafiri kwangu, pia. Nafikiri mara ya mwisho nilipokuwa hapa Lakeport ilikuwa baridi kupita kiasi. Nitawasili wakati mzuri wakati mmoja, kama nikiendelea tu kujaribu. Katikati ya haya yote nina furaha hata na zaidi kusema nina furaha kuwa hapa Lakeport tena usiku wa leo. Tangu niliposikia ya kwamba ninakuja, mbona, nimeutazamia wakati huu.

² Mji mdogo, huku nyuma kabisa milimani, lakini baadhi ya watu wazuri sana niliopata kukutana nao maishani mwangu, wazuri tu, kile ninachoita, watu wanyenyekevu kabisa. Na kufanya ushirika kama huo pamoja na watu kama hao, inanifanya nijisikie vizuri sana.

³ Nanii...Ndugu Folst alikuwa tu akiniambia...Jana jioni nilipoingia, mbona, nilikuwa...moteli ya kwanza niliyofikia, mbona, niliwaza, “Hapa ndipo mahali nitakapokaa.” Na kwa hiyo nikaingia, bila shaka palikuwa ndipo, nami nikatia sahihi ile kadi ndogo pale kwamba nitakaa pale. Basi nilipoamka asubuhi ya leo niliwaza, “Vema, afadhali nishuke niende nione mahali hapa panagharimu nini.” Niliposikia gharama yake, nilibadilisha mahali mara moja. Ndugu Folst ndiyo kwanza aniambie, kasema, “Lakini tunataka ustarehe.”

⁴ Nikasema, “Ndugu, kwa gharama kama hiyo, afadhali nipige kambi chini ya mwerezi hapa nje.” Naam, bwana. Mimi...Haidhuru, kama watu wa kanisa wako tayari kupalipia, si Ukristo ku—kufanya mambo kama hayo. La, bwana. Afadhali niwe na mahali padogo sa—safi tu, na hilo tu ndilo linalohitajika, kuliko kuchukua kitu kinacholilazimu ka—kanisa kulipa kitu kama hicho. La. Si—si—sipendi hilo kwa Wafanyabiashara Wakristo, hasa.

⁵ Ninataka kuwasalimu na kusema hakika ninafurahia hilo, ninashukuru kwamba Bwana amenipa kibali kwao kwamba wangenikaribisha tena. Hii kwa namna fulani tukio sambamba lisilopangwa, nadhani, ninapaswa kuwa Ujerumani sasa, nami, katika hali ngumu, nisingeweza kuondoka kwenda ng'ambo, kwa hiyo ilinibidi kuchukua mwezi huu na mwingine kwa ajili ya ibada. Nami nimekuja tu hapa kuwatembelea ninyi watu wazuri hapa, kuwaombea wagonjwa, na kuhudumu, na kuona kama ninaweza kumfanya mtu kumkubali Bwana wetu mpendwa Yesu.

⁶ Ndio kwanza nipate ono, ama, jambo fulani lilinipata majuma machache yaliyopita, labda baadaye kidogo katika ibada ninaweza kuwaambia habari zake. Na sijawahi kujisikia

vivyo hivyo na sitajisikia vivyo hivyo kulihusu tena. Mimi, natumaini sifanyi kama mlokole, bali nina hakika ya kwamba niliiona Mbingu. Wala si—sitaki kamwe kuikosa hiyo, nami ninataka kumfanya kila mtu niwezaye aende huko.

⁷ Da—daima nimeninii, kulikuwa na hofu kidogo ya yale yatakayonipata kati ya wakati nitakapokufa, na halafu kuja kwa Yesu, daima nilifikiri ningekuwa na mwili wa roho. Kamwe sikupenda chochote cha kimizuka namna hiyo, kamwe siwezi kuvumilia kitu hicho. Kwa hiyo mimi . . . Daima kiliniogopesha.

⁸ Lakini hivi majuzi asubuhi nyumbani kwangu jambo fulani lilitukia, na mke wangu pale, na watoto wangu, na kadhalika, wala sikuenda mbali sana, mbali tu kidogo, nami nikaona, kihalisi, mamilioni ambao nimewahubiria, wote wakiwa wachanga na wenye afya, wala hawatakufa kamwe, nao wakanikumbatia. Ndipo nikaangalia nyuma na kujiona nimelala kitandani, ndipo ni—nikawazia, “Hii ni . . . ?” Ilikuwa ni kamilifu kabisa, ni *kitu fulani* tu.

⁹ Mimi, nilipojua kwamba ilinibidi kurudi, nilisikitika sana, nikasema, “Hakika si lazima niondoke sasa.” Na watu niliowajua walikuwa wameokoka wakiwa na umri wa karibu miaka tisini kabla hawajaokoka, walikuwa vijana, na warembo, na wakiniita ndugu yao.

¹⁰ Mimi, kama hivyo ndivyo ilivyo ni—niko tayari kwenda wakati wowote, hakuna wasiwasi. Lakini basi nilitambua kile Biblia ilichomaanisha wakati iliposema, “Nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine inayongoja tayari.”

¹¹ Kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake, marafiki, hiyo ni kweli. Popote pale ilipokuwa, sijui kama nilikuwa katika mwili huu, ama kama nilikuwa nje yake, simaanishi kumwiga Mtakatifu Paulo mashuhuri, bali popote pale, Mungu na ajalie ya kwamba kila mmoja wenu atakuwa huko. Si—si kitu ambacho sijawahi kuona, wala kuwa na ono lolote, ama chochote kama hicho, kiliyabadilisha tu maisha yangu.

¹² Kijana mwanamke mrembo aliyesimama pale alikuwa ndiyo kwanza anisalimie na kuniita ndugu yake wa thamani.

Nikasema, “Sielewi hili.”

¹³ Kasema, “Alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo.” Kasema, “Hatazeeka tena, hatakuwa . . . hatawahi kufa, kamwe hatashikwa na ugonjwa,” kasema, “hiyo ndiyo sababu alisema, ‘ndugu wa thamani.’”

¹⁴ Loo, laiti ningalibaki tu huko milele! Ninii tu, hamna jana, hamna kesho, uko—uko tu hapo. Wala hakuna—hakuna dhambi, hakuna dhambi inayoweza kutukia, dhambi haiwezi kuweko. Na kila kitu kilikuwa ni upendo mkamilifu. Kama ningejaribu kusema ilikuwa ni ukamilifu, hilo halingelikidhi,

adhimu, hilo halingelikidhi, kamwe sijui, sina maneno yoyote nijuayo katika lahaja ya Kiingereza ku—kuelezea vile Mahali hapo palivyokuwa. Sijawahi kuona, wala kusikia, wala kuwazia chochote kama hicho.

¹⁵ Sasa, labda ilikuwa ni ono. Sijawahi kuwa na ono kama hilo, kati ya mamia ya maelfu ya maono ambayo nimekuwa nayo, sijawahi kuwa na chochote kama hicho, maana nilikuwa nimesimama Mahali fulani hapa, na ningeangalia nyuma na kuona mwili wangu umelala pale kitandani kando ya mke wangu. Ilikuwa saa tatu, ama saa nne, saa mbili, ama tatu asubuhi. Nami ningeangalia nyuma na kupaona, nami ningendoka kwenye kitu fulani, nami nilifikiri nilikuwa nimekufa, na kwa umbali wa kutosha ningeweza kuuona.

¹⁶ Nikiangalia jukwaa hili kwa baadhi ya marafiki zangu walio hapa, mmoja wa mashemasi wa kanisa letu, ama wadhamini, hasa, Ndugu Sothmann na hao wengine, ile picha iliyopigwa, ilipigwa papa hapa kwenye jukwaa hili mara ya mwisho nilipokuwapo. Ni wangapi wamewahi kuiona? Mnamaanisha si...? Loo, wachache tu, watu tu kutoka moja kwa moja nyumbani. Loo, ni moja ya zile maarufu sana, Malaika yule yule wa Bwana ambaye amepigwa picha kote Ujerumani, na kila mahali, alipigwa picha amesimama papa hapa kwenye mimbara hii.

¹⁷ Ilitokea niliona maua haya hapa, kulikuwa na kitu kama hicho kimewekwa hapa mbele, yule mtu akipiga picha upande huu, na Hiyo hapo, kamilifu tu, Bwana wetu, iwezavyo kuwa.

¹⁸ Na kwa hiyo tuna furaha sana kurudi mahali hapa padogo tena usiku wa leo. Sasa, sitaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi, maana najua kuna joto huko nje. Wala sitaki kuwaweka muda mrefu kusudi iwachoshe, na hata hivyo ninawazia kwamba labda, Bwana akipenda, huu ndio wakati ambapo kuna huduma mpya inayokuja mbele kwa ajili yangu, nami, labda, natumaini ya kwamba itaanzia hapa. Hata hivyo, nitajaribu, kwa moyo wangu wote, kuwaombea wagonjwa jinsi alivyoniambia katika mkutano huu.

¹⁹ Kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu. Hujawahi kuwa...Loo, jamani! Itanibidi kubadilisha somo langu. Kuna wengi sana hapa ambao hawajawahi kuwa kwenye—kwenye mikutano yangu hapo kabla, hawajawahi kuwa, vema, basi afadhali nirudi kwenye huduma ya kale usiku wa leo, halafu basi huduma mpya ianze kesho jioni.

²⁰ Hivi vitabu vidogo hapa ndani kwa namna fulani, walivyo navyo hawa wavulana, vinaielezea, kama ungeweza kujipatia kimoja. Na kama una...Nafikiri wao huviuza vizuri, vinachapishwa na *Sauti Ya Uponyaji*, na halafu vinaninii, tunavichukua na kuvileta kwa watu, tunavinunua kwa

senti arobaini pungufu kwenye vitabu, asilimia arobaini pungufu, kisha tuna gharama ya kuvishughulikia mbali na hiyo. Tunavilipia kuuzwa na kubebwa, na kuna uchukuzi na gharama; sikuzote tunaenda hasara kwa kitabu.

²¹ Halafu sikuzote tunasema hivi, ya kwamba kama mtu yeyote akitaka kimoja, hana pesa, nimewaomba hao wavulana, wawaachie, kwa vyovyote vile, wawape tu. Kama ukiwahi... Ukikipata na kukisoma, hakina thamani ya senti hamsini, chochote ulichokilipia, ninasahau tu kwamba ni ngapi, basi kirudishe tu, urudishiwe pesa zako, ama, ukiweke na uwaambie hakikuwa kizuri, kwa hiyo basi tutawarudishia pesa, kwa vyovyote vile. Ni kwa njia fulani tu, hatuna kitu cha kuuza, ambacho, cha kutupatia pesa. Hao wavulana wanauza kanda, nazo ni rahisi tu iwezekanavyo.

²² Mimi, kabla sijawaruhusu kufanya hivyo, niliwasiliana na mwinjilisti mwingine, alikuwa akipata dola tisa kwa kanda, naamini, alinilipisha hizo. Halafu basi wavulana hawa, nafikiri wanaziua kwa dola mbili ama kitu kama hicho, kwenye kanda bora zaidi. Zimehakikishiwa, pia, kama haifai kitu, mbona, sio lazima uzilipie. Zile jumbe, jumbe mbalimbali mia tano na kitu zimehubiriwa hivi punde katika sehemu mbalimbali nchini.

²³ Kama sijakosea, hivi ninamwangalia Jack Palmer kote huko kusini? Ndugu Jack, kwani unafanya nini huku juu kabisa? Hukuwa kwenye mkutano wa mwisho, sivyo? Jamani, jamani! Mtu huyo anatoka huko mbali sana kusini mwa Georgia. Nafikiri tunapaswa kusema, "Bwana asifiwe." Je, kuna joto hivi huko Georgia? Hamna. Ni unyevu zaidi tu kidogo hewani. Vema, hawa watu wa California hawaujali, wameuzoea.

²⁴ Sasa, ni wangapi hapa ndani walio Wakristo? Hebu tuone mikono yenu, mnaompenda Bwana. Loo, angalieni hapo, ninaamini asilimia mia moja. Ninafurahia hilo sana.

²⁵ Sasa, kama... Nitakuwa na somo la Maandiko na kuzunguma kidogo usiku wa leo, halafu nita—nitaagiza mstari wa maombi nasi tutawaomba jinsi tulivyokuwa tukifanya, halafu labda kesho usiku tutaanza ile huduma nyingine.

²⁶ Sasa, Bwana akipenda, nataka kuomba, kama mtashikilia tu pamoja nami, nitamwomba kila mtu anayekuja hapa anayetaka kuombewa, mnaona, kila mtu, hatutamwacha hata mmoja, mnaona, tutamwomba kila mmoja.

²⁷ Kile tunachojaribu kufanya... Uponyaji wa Kiungu haumaanishi kwamba nguvu fulani kuu, kwamba mtu hana budi kumponya mwingine, bali ni imani katika kufufuka Kwake Yesu Kristo, endapo tunaweza kuamini ya kwamba Yeye hajafa, bali yu hai. Halafu mada ya uamsho wetu sikuzote ni Waebrania 13:8, "Yesu Kristo *yeye yule* jana, leo, na hata milele."

²⁸ Ni wangapi wenu ninyi Wakristo wanaoamini hilo, ya kwamba Yeye ni yule yule jana? Asanteni. Hiyo inamaanisha

ninyi ni Wakristo halisi, mnapoamini hilo. Sasa, Yeye hajafa, bali Yu hai.

²⁹ Nimekuwa kote ulimwenguni, na katika mahali pa kila namna, na chini ya mazingira ya kila namna, dini za kila namna, Hivi majuzi nilikaribishwa na dini kumi na saba mbalimbali, na kila moja yao iliukanusha Ukristo, na hata hivyo, miongoni mwa watu laki tano ambao nilikuwa nikiwazungumzia huko Bombay, Bwana Yesu Kristo na Ukristo walishinda kila moja yazo ikaaibisha kila mchawi, na mtu mtakatifu, na kila kitu kingine. Wala hakuna njia ya kusema ni wangapi waliomjia Bwana Yesu, hatukuwa na ushirikiano miongoni mwa makanisa, na tuliingia mle kwa siku tatu pekee, wala hapakuwapo na njia ya kusema ni wangapi waliookolewa.

³⁰ Sasa, tutainamisha tu vichwa vyetu sasa, na kumwendea Mungu pamoja na Neno. Sasa, tutakumbuka ya kwamba ninii, kila tufanyacho kinaninii, na kufundisha lazima kiwe na msingi juu ya Biblia hii, kimetambulishwa kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo.

³¹ Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha usiku wa leo kuwa Wakristo. Kamwe sijui ningefanya nini kama sikuwa Mkristo, nina furaha sana kwamba Wewe uliniokoa.

³² Na hivi majuzi, chochote kile kilichonipata, nami nikaona matokeo hayo makuu wakati Yule aliyekuwa akizungumza nami aliposema, “Hawa ni waongofu wako kutoka kwenye ninii ya—yako, tunda la huduma yako,” jinsi moyo wangu ulivyoruka!

³³ Nami nikawazia, “Ee Mungu, kama ningeweza kuyaishi tena, ningejaribu kufanya mara mbili zaidi. Ningewashawishi na kuwasihii kwa yote yaliyo ndani yangu kuwafanya watu waje Kwako.”

³⁴ Sasa, Baba, hapa usiku wa leo kuna nafasi nyingine, walionunuliwa kwa Damu Yako wako hapa mbele yangu. Basi unisaidie, Baba Mungu, kama mtumishi Wako, sijui la kufanya wala jinsi ya kulifanya, ninakutegemea Wewe uniongoze saa baada ya saa. Nao wameketi hapa, sio tu waonekane katika hali hii ya joto usiku wa leo, wamekuja kwa sababu fulani, wanaona njaa na kiu, wanakupenda, wengi wao ni wagonjwa na wanakufa, wengine wanateseka.

³⁵ Jalia tusicheze tu sasa, bali jalia tuzame moja kwa moja kwenye unyofu wa Neno, katika Injili, na kuomba kwa yote yaliyo ndani yetu, tufunge na kukungojea Wewe, na kujua ya kwamba Wewe utafanya mambo ya ajabu mno, kwa wingi, zaidi ya yote tuwezayo kufanya au kuwazia, laiti tungejikabidhi tu Kwako, na kukusudia moyoni mwetu, kama alivyofanya Danieli huko Babeli, kwamba hatutajitia unajisi kwa kutokuamini, bali tutamwacha Roho Mtakatifu aondoe kutokuamini kwote kutoka kwetu, na kumwamini Yeye kwa mioyo yetu yote.

36 Tunalikaribia Neno sasa hivi, nena nasi, Baba, kupitia Neno Lako. Kwa kuwa ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

37 Nawatakeni mfungue, usiku wa leo, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, na hebu tufungue mlango wa 14, mkiweza, katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, ninataka kuanza kusoma kwenye kifungu cha 22:

Mara Yesu akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni, na kutangulia kwenda ng'ambo ya pili, wakati Yeye alipokuwa akiwaaga makutano.

Naye alipokwisha kuwaaga makutano, alipanda mlimani faraghani kwenda kuomba: na kulipokuwa jioni, alikuwa huko peke yake.

Basi kile chombo sasa kimekwisha kufika katikati ya bahari, kinataabika sana na mawimbi, maana upepo ulikuwa wa mbisho.

Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaenda, akienda kwa miguu juu ya bahari.

Wanafunzi walipomwona akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.

Mara Yesu. . . Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipemi moyo; ni mimi; msioope.

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

38 Ninataka kuchukua kwa ajili ya somo, kutoa muktadha kutoka kwenye kifungu hicho cha 27: “Msioope, Ni Mimi.” Nayo maneno ninayotaka kutumia ni *Ni Mimi*.

39 Hapana shaka ilikuwa yapata wakati huu wa jioni, jua linatua tu wakati kila mmoja wao alipochukua mahali pake kwenye—kwenye kishwara mashuani mwao. Nayo maskini ile bahari, kama nilivyokuwa nimeketi alasiri ya leo, nikiwazia nilipokuwa nikiangalia ng'ambo ya ziwa, hapana shaka ilikuwa kitu kama hicho, Galilaya ina ukubwa kama huo, na labda pana zaidi kidogo.

40 Ndipo yule mvuvi mkubwa na misuli yake migumu, mikubwa, akaanza kuusogeza huo mtumbwi, huku akiisukuma gu—gubeti ziwani. Akipanda juu ya hao mitume wengine, na kuinua miguu yake kuelekea mbe—mbele ya mashua, akaketi chini, labda, karibu na ndugu yake, Andrea, na marafiki zake wazuri.

41 Na hasa katika ushirika wa Kikristo, kuna jambo fulani kuhusu wakati umekuwa na kundi la watu mahali alipo Yesu, ni vigumu sana kuachana na watu hao. Kuna kitu kinachotuunganisha tu pamoja, tunapoketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu. Ni hisia ya jinsi gani kwa watu

kukusanyika pamoja katika ushirika huo pamoja na Bwana Yesu!

⁴² Hilo ndilo walilokuwa wamefurahia siku hiyo. Na maelfu walikuwa wamesimama ukingoni, watu elfu tano au zaidi, nao walikuwa wakiwapungia mkono kwaheri. Na kama ilivyo kwa ushirika, ni vigumu kwetu kuachana.

⁴³ Nasi tulikuwa tukiwazia juu ya ule wimbo wa kale tuliokuwa tukiimba kanisani miaka mingi iliyopita nilipokuwa nikichunga maskini ile maskani ya Kibaptisti mjini mwangu, Jeffersonville, Indiana, tulikuwa tukiimba wimbo huu wa kale:

Kibarikiwe kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko Juu.

Tunapoachana,
Inatupa maumivu ya ndani;
Lakini bado tutaungana moyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

Wengi wenu mmeusikia wimbo huo wa kale, ni wimbo maarufu, wa kale wa kanisa, ambao umependwa sana kwa miaka mingi.

⁴⁴ Basi walipokuwa wakiwapungia mkono kwaheri wale waliokuwa ukingoni, huku maskini ile meli ikielea kwenye maji baharini, giza lilianza kunyemelea kutoka ng'ambo ya pili kuelekea Gadara, nao walikuwa, huku kivuli kikianguka majini, ile meli ndogo ilikuwa karibu haionekani kwa wanafunzi, ama, watu waliokuwa ukingoni, wakati wanafunzi walipoingia ziwani.

⁴⁵ Ninaamini hapana shaka ilikuwa ni muda mwingi kweli, labda niseme dakika kumi kabla mtu yeyote hajasema maneno mengine, huku maskini ile meli imechukuliwa na mkondo, na kila mtume, akiwa na ka—kasia, ninii tu, na kuzunguka tu kwa wakati unaofaa.

⁴⁶ Na hapo tunajifunza somo, pia: Kwenye meli hii ndogo inayosafiri juu ya barabara kuu ya maisha, tunayoendelea nayo, kama tu tukiungana pamoja, meli itasonga vizuri zaidi. Kama Baptisti, na Presbiteri, na Pentekoste, Assemblies of God, na Church of God, na wote, wataungana tu, maskini hiyo meli hakika itaabiri vizuri.

⁴⁷ Na walipokuwa wakiisogeza maskini ile meli ndogo kuelekea pwani ya pili, kikomo chao, hapana shaka ilikuwa ni yule kijana Yohana, alikuwa ndiye mdogo kuliko wote miongoni mwa kundi hilo, ambaye alizisukuma nyuma nywele za matimutimu usoni mwake, na kungoja kwa muda kidogo tu huku ametulia juu ya makasia yake. Hao ndugu wakangojea na kushangaa alichokuwa anaenda kusema. Ndipo hapana shaka aligeuka na kitu kama

hiki, na kusema, “Ndugu zangu, nimeshawishika hata na zaidi, usiku wa leo, ya kwamba hatufuati namna fulani ya mshupavu wa dini. Nina hakika zaidi kuliko nilivyowahi kuwa maishani mwangu mwote ya kwamba tunamfuata Mwana wa kweli wa Mungu. Nilishawishika zaidi leo kuliko hapo kabla.

⁴⁸ “Kama mvulana mdogo, nilipenda kumsikia mama yangu akisoma habari za Yehova mkuu, Ambaye alikuwa Mungu mwenye nguvu, Ambaye angeweza kufanya miujiza, na kunena mambo yakawa, na kuumba kwa Neno Lake Mwenyewe. Naye mama yangu alizoea kuniambia, ‘Mwanangu, vitu vyote viliumbwa na Mungu, Naye alivinena tu vikawa.’

⁴⁹ “Ndipo basi nilikuwa ninapenda kusikia hadithi hiyo, wakati watu wetu wa kale walipotoka Misri, miaka arobaini nyikani, jinsi Yehova alivyowaongoza. Ndipo walipoona njaa, Yehova alimimina tu mkate kutoka Mbinguni. Na kama mvulana mdogo nilikuwa nikiwazia, jinsi ambavyo ningetaka Yehova amimine baadhi ya chakula hicho cha Malaika sasa, kwa sababu ilisema, ‘Ilikuwa mikate myembamba pamoja na asali,’ nami ningefurahia kuipata.

⁵⁰ “Nanyi mnajua siku hizi, nilipomwona akiwachukua wale samaki watano, ama, mikate mitano na samaki wawili wadogo, na kuwalisha watu elfu tano, nilijua hapana shaka huyo alikuwa ni Yehova, Najua hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya hivyo.

⁵¹ “Na, ndugu, nilitambaa karibu na jiwe hilo, nilipomwona mvulana huyo mdogo, ambaye sisi... aliyetufuata huko chini asubuhi ya leo, alikuwa ametoroka shuleni, yeye na dada yake mdogo, naye alikuwa na chakula hiki cha mchana chini ya mkono wake, basi nilipomwona Petro pale akimwuliza kuhusu chakula hicho cha mchana wakati kila mtu alikuwa na njaa, nacho kikawekwa mikononi mwa Bwana wetu, niliwazia jinsi kilivyokuwa chakula cha kutosha mle ndani kumlisha maskini mvulana huyo chakula chake cha kutwa. Lakini kilipokuwa mikononi mwa Yesu, kingeweza kuwalisha watu elfu tano na viokotwe vikapu kadhaa vilivyojaa vipande.”

⁵² Jinsi Mungu anavyoweza kuzidisha kile tunachoweka mikononi Mwake! Mikononi mwetu sio kingi, mikononi Mwake anakizidisha kwa maelfu. Laiti tungeweza kumwacha achukue kidogo tulicho nacho, wakati wetu, usikivu wetu, imani yetu huenda isiwe nyingi sana, kama vile dada yetu aliyeketi hapa, huyu aliyeshika mkongojo na mwingine ameketi kwenye kiti cha magurudumu, na mtu wa thamani aliyeketi akiniangalia pale, akiwa na mkongojo na kiti cha magurudumu, huenda isiwe, imani kidogo uliyo nayo huenda isiwe nyingi sana, lakini kama ingeweza tu kuingia mara moja mikononi mwa Kristo, kile Yeye angeweza kufanya nayo! Hivi viti vya magurudumu

vingesukumiwa ukutani, washuke waende mitaani kesho wakimsifu Mungu, wakimshukuru Mungu.

⁵³ Wengi walioketi hapa, wakifa kwa ugonjwa wa moyo, kansa, chochote kile, katika siku chache tangu sasa huenda ukarudi kwa daktari wako, naye angesema, “Aisee, imekuwaje hapa?”

⁵⁴ Ni kitu gani? Kile kidogo ulichokuwa nacho, ulikikabidhi mikononi mwa Kristo Naye akaanza kukizidisha, kansa ikaanza kutoweka, moyo ukaanza kurudi mahali pake panapofaa na kudunda moja kwa moja tena. Mwache tu akishike mkononi Mwake.

⁵⁵ Akasema, “Nilipomwona akichukua hizo biskuti tano na—na samaki wawili na kuwavunja, nilipanda juu ya mwamba na kuchungulia nione jinsi alivyofanya hilo. Nami ningekiona hicho kipande cha samaki mkononi Mwake, angekivunja na kukiweka *hapa*, ndipo alipounyosha mkono tena, kungekuwako na samaki mwingine pale, sio samaki tu majini, bali samaki tayari amekuzwa, na kupikwa, na yuko tayari, tayari kwa kuliwa. Ndipo nilipomwona akiumea maskini mkate huo vipande viwili, akauweka hapa, ila alipounyosha mkono tena kulikuwako na mkate mwingine tayari kumegwa tena.”

⁵⁶ Loo, jinsi angeweza kuikuza mikate! Ninataka kuuliza, kama kungekuwako na mwanasayansi hapa, “Ni atomu ya namna gani Yeye alifungulia wakati huo kufanya ngano ya kawaida, bila shaka?” Ilikuwa ni ile ile aliyoiachilia wakati alipoyageza maji yakawa divai.

⁵⁷ Yeye ni Mungu, Yeye hufanya atakalo. Naye yuko tayari kufanya mambo yote na kutupatia mengi, kwa wingi, kuliko hata tuwezavyo kuwazia ikiwa tutajiachilia tu tufanywe huru kwa imani katika Yeye; hapo ndipo lilipo, ni kumwamini Yeye kuamini kwamba anaweza. “Kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio,” haijalishi ni nini, inawezekana. Na si kwamba tu inawezekana, yamkini, na itatendeka, kama tu utaamini.

⁵⁸ Sasa, basi kijana Yohana, alipoangalia kule chini, na kusema, “Niliona basi ya kwamba Yeye alifanya jambo fulani, alifanya jambo kama vile Yehova alivyolifanya. Nami nikamsikia akisema, ndugu, ya kwamba ‘Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, nanyi hamwezi kuniamini Mimi, basi ziaminini hizo kazi.’”

⁵⁹ Jinsi hilo lilivyo kamilifu! Jinsi hilo linavyotumika kwa wakati wowote! Maadamu Yesu yu hai usiku wa leo, Yeye ni Mungu tu usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo, vile vile tu. Mnaona?

⁶⁰ “Kasema, ‘Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu,’” kijana Yohana hapana shaka alisema, “Nilisoma katika Biblia ambapo Yehova angeweza kufanya mikate itoke Mbinguni, angeweza

kuumba mikate Mbinguni, na kuituma duniani, na, ndugu, mkate huo ilibidi utoke Mbinguni, kwa sababu nilimwona akiumega na kuusambaza. Nami nimeshawishika kwa yote yaliyo moyoni mwangu, ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu aliye hai.” Naam.

⁶¹ Jinsi hapana shaka alisema hivyo huku machozi yakitiririka kwenye mashavu yake machanga! Kamwe hakulisahau. Kamwe hakulisahau, alipokuwa mzee ingebidi kubebwa awekwe jukwaani, ahubiri mahubiri mafupi tu waliyosema ni ya yapata saa nne, kwamba, yeye, bado ulimshurutisha, upendo huo ambao yeye, yote aliyoweza kuzungumzia yalikuwa, “Watoto wadogo, pendaneni,” kulirudia tu tena, “watoto wadogo, pendaneni, kwa maana yeye apendaye ni wa Mungu, kwa kuwa Mungu ni upendo,” kwamba inahitaji upendo halisi kuumba.

⁶² Upendo, hebu mkeo ajue kwamba unampenda, yeye anakupenda, itaninii, wakati mkiwa mume na mke vijana na mmepata kibali mmoja kwa mwingine, inawafanya muungane pamoja kwa ajili ya safari ya maisha, upendo. Na huo ni upendo wa fileo, huo ni upendo wa kibinadamu, upendo wa Agapao utafanya nini wakati kweli unaweza kuingia mahali fulani ambapo unaweza kumwonyesha Mungu ya kwamba unampenda na unamwamini Yeye? Jinsi utakavyojiunga Naye, si kwa ajili ya safari ya maisha tu, bali kwa ajili ya Umilele! Jinsi ulivyo tayari kulichukua Neno Lake, kwa yale tu Yeye asemayo, na kusema, “Hilo ni la kweli, Bwana, silitili swali,” endelea moja kwa moja! Hilo ndilo linalohitaji upendo halisi.

⁶³ Naye kijana Yohana, alipokuwa ameketi pale huku ameweka mikono yake imetulia juu ya makasia, labda basi mtu mmoja aliyashika makasia nao wakaanza tena. Giza lilikuwa linaingia sasa.

⁶⁴ Ndipo basi, baada ya kijana Yohana kupata nafasi yake ya kusema, hapana shaka ilikuwa ni mtume, Petro, yule mvuvi mkubwa, mwenye misuli migumu aliyeketi kuelekea ule mtumbwi, kwenye shetri ambapo ndiyo kwanza asukume gubeti nje, na kuruka kwenye shetri, akaketi karibu na ndugu yake Andrea, hapana shaka alisimama apate ninii yake . . .

⁶⁵ Mwajua, sote hatuna budi kuwa na ushuhuda mdogo mara kwa mara, tunapokusanyika pamoja. Bado ninaupenda (Nanyi je?), mkutano mzuri wa ushuhuda.

⁶⁶ Na kwa hiyo, hapana shaka ilikuwa ni mtume Petro ambaye asingeweza kujizuia tena, basi akasema, “Vema, ndugu, na—nataka kushuhudia, pia. Wakati Andrea hapa, ndugu yangu, alipokuwa amepanda kwenda kumtembelea huyu, *anayejiita* Nabii wa Galilaya, ilivyokuwa ikienezwa, nilikuwa nimemsikia kuhani wangu akisema hekaluni ati ni bure kwa sababu Mungu hakuwa na manabii wengine, na—nami nilikuwa nimesikia

uvumi wa kila namna wa uponyaji, na kadhalika, lakini ni—nisingeweza kuamini hilo.

⁶⁷ “Lakini siku moja tulipokuwa tukiosha nyavu zetu Jamaa huyu alishuka akaja u—ufukoni kuhubiri, ndipo nikajiokotea kisiki nikarudi kando ufukoni, nikaketi chini. Lakini alipoanza kunena, kulikuwa na jambo *fulani* kumhusu Yeye ambalo lilikuwa tofauti na kasisi yeyote au mhubiri niliyepata kumsikiliza.”

⁶⁸ Na, ndugu, wakati unapoketi kimya vya kutosha na kusikiliza, mpaka unaweza kusikia Sauti hiyo ndogo tulivu ya Kristo, ni tofauti na ujumbe wowote uliowahi kusikia maishani mwako. Inaleti amani, inaleti utoshelevu, inakufanyia jambo *fulani* linalochochea utu wako wa ndani kabisa, wewe si yeye yule tena. Mwanadamu hawezi kukutana na Mungu na kuzungumza na Mungu, na kamwe abaki vile vile tena.

⁶⁹ Sasa, yeye akasema, “Lakini wakati. . . Nilikuwa nayo yote moyoni mwangu.” Kasema, “Baada ya kumjua baba yangu mzee mtauwa, ambaye alikuwa ni Farisayo, kama vile ninyi ndugu mnavyojua ya kuwa yeye alikuwa ni Farisayo, ndipo basi, alipokuwa anazeeka, ninakumbuka jinsi alivyokuwa akiketi akiisha kuvua samaki siku nzima kwenye ziwa hili, angeketi chini pembeni kule, mahali tulipozoea kuingiza nyavu, siku moja alinichukua mikononi mwake na kuniambia, ‘Simoni, mvulana wangu mdogo, itambidi Baba akuache moja ya siku hizi, nikukabidhi yote, mashua yangu, na vyombo vya kufulia, na kadhalika, nikuachie wewe.’”

⁷⁰ Ninapomwangalia mvulana wangu mdogo, Joseph, na kuwazia jambo lile lile, siku moja sina budi kumkabidhi Biblia, na yote ni—niliyo nayo.

⁷¹ Naye akasema, “Huku baba yangu akisukuma mvi kutoka kwenye paji la uso wake, na ndevu zake nyeupe, alisema, ‘Simoni, keti chini, nataka kukushauri, mwanangu. Miaka yote tumengojea, watu wetu wamemngojea Masihi ajaye. Na sasa tumejibunia maelezo mengi, na, ya jinsi atakavyoonekana ajapo, akishuka kutoka Mbinguni, sasa, katika gari, likiendeshwa na Malaika, ama farasi, ama chochote kile, tuna maelezo mengi, bali Simoni, huyo hatakuwa Masihi ajaye. Masihi ajapo, Yeye atakuja kwa njia tofauti na vile yeyote wa marabi wetu anavyowazia.

⁷² “Sasa, Simoni, ninataka usome Maandiko, maana Maandiko daima yanasema kweli. Sasa, hili hapa jambo moja unaloweza kukumbuka: Atakapokuja, Yeye atakataliwa, Yeye atakuwa Mtu aliyekataliwa, kwa sababu kila Ujumbe wa kweli wa Mungu sikuzote unakataliwa, daima umekataliwa, daima utakataliwa. Utakataliwa na wi—wingi wa watu, wataukataa.

⁷³ “Sasa hapa ndipo utakapopata: Huenda kukatokea Masihi wengi wa uongo kabla ya wakati wako, Simoni. Daima nimewazia ya kwamba ningeishi nipate kumwona Yeye. Lakini

ninazeeka, na labda sitamwona. Lakini, Simoni, kamwe usiache jambo hili likuondokee, Masihi ajapo, Yeye atakuwa ni Nabii, atakuwa ni Mungu-Nabii, kwa sababu, Simoni, Musa, yule tunayefuata maagizo yake sasa, alisema katika neno lake, ambapo yeye alikuwa ni nabii, alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Na sasa ukumbuke ajapo Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii kama Musa, bali Yeye atakuwa zaidi ya Nabii, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii, itakuwa ni Mungu katika Nabii, akijidhihirisha Mwenyewe.

⁷⁴ “Na utakapoona ile ishara kuu, sasa, watu wakiinuka na kusema wao ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*, usiamini hilo, Simoni, lakini utakapomwona Mungu akitenda ishara ya nabii, kwa sababu hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi, itakuwa ndiyo ishara ya nabii, kwa sababu Musa alisema, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi, Mtoa-Sheria, Kuhani, Mfalme, Nabii. Na itakuwa kwamba mtu yeyote asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na, miongoni mwa watu.”

⁷⁵ “Isaya alisema angekataliwa, Mtu wa huzuni, ajuaye sikitiko, tungeficha, kama ilivyokuwa, nyuso zetu. Sasa, usiuamini mwelekeo Wake wa kisasa, Simoni, bali angalia ishara hiyo ya Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii.’

⁷⁶ “Basi enyi ndugu, siku hiyo tukiketi kwenye kisiki,” yeye alisema, labda, kwa mitume tunapousimulia maskini huu mchezo wa kuigiza, “Niliketi pale na kumtazama na kumsikiliza Mtu huyu, Yeye alikuwa m—Mnenaji hodari sana, hakuzungumza kama mmoja wa makuhani kutoka kwenye Biblia, kutoka kwenye Magombo, Yeye alinena kwa nguvu. Na wakati aliponena, alionekana kuwa na matumaini kamili yale aliyosema yalikuwa sahihi, kwa hiyo kidogo nikaanza kumpenda.

⁷⁷ “Ndipo kwa ghafla, Yeye akageuka na kuniangalia nimeketi kwenye kile kisiki, na kusema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Hilo lilinithibitishia ya kwamba Yeye Ndiye atakayetumwa na Mungu, alikuwa ndiye yule Mungu-Nabii. Kwa kuwa Yeye hakunijua tu, kwamba jina langu lilikuwa Simoni, bali alimjua yule baba yangu mzee mtauwa. Akasema, ‘Wewe ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,’ baba yangu, kwa hiyo, nilijua ya kwamba baba yangu alikuwa amenifundisha kwa Biblia, na sasa Biblia ilikuwa ni kweli iliyo hai kwamba hapa Yeye alikuwa akiniita kwa jina, ambaye hata hajawahi kuniona maishani Mwake.

⁷⁸ “Hajawahi kusikia habari zangu, hakujuu lolote kunihusu mimi, na hapa Yeye ananiita Simoni, isitoshe, bali alinena juu ya baba yangu mzee ambaye ameondoka kwa miaka hamsini, kasema, ‘Wewe ni mwana wa Yona.’ Aliposema hivyo nilianguka

miguuni Pake, maana nilijua Huyu alikuwa ndiye Masihi.” Amina.

⁷⁹ Masihi jana. Masihi angekuwa nini leo kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele?

⁸⁰ Vema, hapana shaka ilikuwa ni yapata wakati huo, zamu ya Filipo, kusimama kwa ajili ya ushuhuda ndani ya chombo, kwa kuwa lilikuwa karibu giza wakati huo, karibu uvuli. Ndipo Filipo akasimama, naye akasema, “Ndugu Nathanaeli, utanishuhudia jambo hili, nilisimama pale na kumwona Bwana wetu akimwambia Simoni hapa, ya kwamba jina lake lilikuwa ni Simoni, alikuwa ni mwana wa Yona, hilo lalinisaidia, pia. Nami nilikuwa na ndugu mmoja aliyekuwa wa dhehebu kubwa lililoitwa Masadukayo, kwa hiyo ni—nikaenda kumwona, na ni kama maili kumi na tano kuuzunguka huo mlima.

⁸¹ “Nilienda huko asubuhi moja, mapema, nikaamka, nikala kiamshakinywa changu, na kuvuka mlima haraka nilivyoweza, ndipo nikaenda kule, na nikafika karibu jioni, ama, hiyo alasiri nikafikia mahali ambapo nilijua kwamba mtu huyu aliishi. Ndipo nikabisha mlango, naye mke wake akasema, ‘Ndiyo kwanza aende kuzuru ki—kijisitu chake, naye yuko huko nje katikati ya miti, mahali fulani. Filipo, utampata huko nje.’

⁸² “Kwa hiyo nikaenda kwenye miti yake, basi nilipofika huko nje nikasikia kelele. Nami nikaenda nikichungulia chini ya mtini, naye huyo hapo amepiga magoti, akiomba.”

Basi huenda alisema, “Unakumbuka hilo, Ndugu Nathanaeli?”

“Amina. Ninakumbuka.”

“Basi nikangojea mpaka alipomaliza kuomba, nami nikamwambia, ‘Njoo, uone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.’

⁸³ “‘Loo,’ akasema, ‘sasa ngoja kidogo. Ni kitu gani hiki unachosema? Sasa, angalia Nathanaeli, ninakujua, umekuwa mtu mwema, nawe umebobea sana Kimaandiko, usijitie uwendawazimu, sasa. Sasa, umefanya nini? Unaniambia ati huyu Nabii wa Galilaya wanayenena habari zake ndiye Masihi?’

⁸⁴ “‘Sikiliza, Nathanaeli, nilimwona, na kumsikia akifanya ishara ya Masihi. Tunajua Masihi anapaswa kuwa Mungu-Nabii. Nami nilimwona akisimama... Unamkumbuka maskini yule mvuvi aliyekuuzia samaki kutoka kule ziwani siku ile, jina lake Simoni?’

“Naam, namkumbuka.’

“‘Alikuwa asiyejua kusoma wala kuandika kabisa, hata asingeweza kutia sahihi risiti ya samaki.’

“‘Ninamkumbuka huyo.’

85 “Mara alipokuja Mbele za huyu Yesu wa Nazareti, Alisema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.”” Akasema, “Sasa, Filipo, ama, Nathanaeli, laiti ungaliweza kuyachunguza Maandiko. Hiyo si ndiyo ishara ya Masihi?”

86 “Naye akasema, ‘Loo, bila shaka Masihi atakuwa ni Nabii, tunajua jambo hilo, tumefunzwa hilo. Lakini tungempata wapi Mtu kama huyo? Je, kuna . . . ? Ametoka wapi?’

“Anatoka Nazareti.’

“Nazareti? Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?”

87 Ninaamini ya kwamba alimpa moja ya majibu mazuri sana ambayo mtu yeyote angeweza kumpa mwenzake, alisema, “Njoo uone.”

88 Hilo ndilo jambo bora zaidi kufanya. Sasa, usikae tu nyumbani na kusema, “Vema, akina Jones walisema *hivi na hivi*.” Usifanye hivyo. Njoo, lete Biblia yako, na uyachunguze Maandiko, uone kama ni kweli ama si kweli. Njoo, ujionee mwenyewe. Usije kwa saa moja tu, njoo ukae mpaka umeshawishika kabisa kwamba ni kweli, hiyo ndiyo njia. Lichunguze kwa Maandiko, ujue kama ni—ni kweli, ama kama si kweli, unaposhawishika kupitia mafundisho ya Maandiko ya Biblia kama ni kweli ama si kweli. Sasa, hilo ndilo alilokuwa akilirejelea, “Njoo ujionee mwenyewe kama kweli ni Masihi ama siye.

89 “Vema,’ akasema, ‘nitakuja nione.’

90 “Kwa hiyo wakati yeye . . . tukitembea barabarani nilimwambia mambo mbalimbali yaliyokuwa yametukia. Na kwa hiyo, wakati alipoenda Mbele za Masihi, kwa Yesu,” Yeye, labda, huenda alikuwa amesimama kama ulivyo wewe, huenda alikuwa ameketi chini, huenda alikuwa jinsi gani . . . hali yoyote aliyokuwamo, “wakati mtu huyu alipoenda Mbele Zake, akiwa ni mtu wa kidini, mtu mwema, Yeye alisema, ‘Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!’

91 “Sasa, jambo hili lilimshangaza, hakujua la kusema basi, alishangaa jinsi alivyopata kujua yeye alikuwa ni nani. Akasema, ‘Rabi,’” ambapo neno *rabi* linamaanisha “mwalimu,” mwalimu wa Kiebrania, “‘Rabi, ulipata kunijua lini? Sasa, Wewe unaniambia hapa ya kwamba mimi ni Mwisraeli.’”

92 Sasa, haikuwa kwa sababu alikuwa amevalia kama Mwisraeli, kwa sababu watu wote wa mashariki, angeweza kuwa ni Mwarabu, au angeweza kuwa Myunani, wote walivaa mavazi, na kilemba, na kama tu wanavyofanya huko mashariki. Angeweza kuwa wa makabila mengi ya watu wakati huo katika nchi ya mashariki. Lakini haikuwa nguo yake, haikuwa ni rangi yake, wote ni weusi, hudhurungi.

93 “Na kwa hiyo Yeye akasema, ‘Wewe ni Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake,’ ushuhuda wa kweli wa moja kwa moja

wa Masihi. Mnaona? ‘Wewe ni Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake.’

“Akasema, ‘Rabi,’” kwa maneno mengine *mwalimu, kasisi*, tungenesema leo, “‘ulipataje kunijua mimi?’”

⁹⁴ “Naye akasema, ‘Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’” Ni macho ya jinsi gani! Maili kumi na tano kuizunguka milima siku iliyotangulia alipokuwa chini ya mti, “Nilikuona.”

⁹⁵ Kisha kasema, “Nikaanguka mbele Zake, nikasema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’” Alijua jambo hilo, alijua kwa sababu aliona ishara ya Masihi juu Yake.

⁹⁶ Basi, hapana shaka ilikuwa ni baada ya yeye kumaliza, ilikuwa ni maskini mzee mwema Andrea akiketi karibu na mtume Petro ambaye alifuata kushuhudia. Hapana shaka ilikuwa ni yeye aliyesema, “Vema, ndugu, hebu nizungumze kwa niaba ya wote. Je, sisi sote hatukushawishika kabisa wakati alipokuwa akishuka kwenda Yeriko kutoka Yerusalemu? Na huo ni mstari mnyofu moja kwa moja chini ya mlima hadi Yeriko, lakini asubuhi hiyo Yeye alisema, ‘Nina haja kupitia Samaria.’ Hiyo ni huko juu ya mlima. Kwa nini imbidi kwenda, kwenda Yeriko, kupitia njia ya Samaria?”

⁹⁷ “Mnakumbuka jinsi sisi sote tulivyojisikia kigeni siku hiyo? Lakini tulikuwa, kila mmoja aliogopa kumwambia chochote, kwa sababu tulijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake, na Mungu alikuwa akimwongoza, wala sisi hatukumwongoza, ha—hatukutaka kusema lolote kulihusu, maana Mungu ndiye aliyekuwa akiongoza.”

⁹⁸ Akasema, “Alikuwa...Tulienda pamoja Naye huko Samaria, nanyi mnakumbuka jinsi maskini mawe hayo... ndipo akachoka sana kupanda huko juu? Basi akaketi kisimani na kututuma huko kununua chakula, huko chini mjini, akaketi karibu na kisima cha umma. Hakukuwako na kitu pale cha kumchotea Yeye maji anywe. Tungemchotea, tulitaka kumpoesha, kwa kumpa maji, na kuoshwa miguu Yake, lakini Yeye akasema, ‘Ndugu, shukeni mwende mkanunue vyakula, nami nitangojea hapa.’” Kitu kama mandhari madogo, mahali kisima kilipokuwa, ni kisima cha umma kwa ajili ya huo mji.

⁹⁹ “Basi tulipokuwa tumeondoka, hawangetuuzia chakula chochote, kwa hiyo tukarudi kisimani. Nanyi mnakumbuka, tulisikia kitu fulani kikiendelea tuliporudi, nasi tukainama kwenye kichaka cha majani pale kusikiliza, tuone yaliyokuwa yakisemwa. Basi kulikuwako na mwa—mwanamke mrembo ambaye tulidhani angekuwa ni mwanamke mcha Mungu sana. Alikuwa ni mrembo, nywele zake, uso wake, naye kidogo alikuwa ni kijana, naye alikuwa akiongea Naye. “Nasi tukamsikia akimwambia, ‘Mwanamke, nipe maji ninywe.’”

100 “Naye akasema, ‘Bwana, si kawaida kwenu Wayahudi kuwaomba Wasamaria kitu kama hicho. Mimi ni mwanamke Msamaria, kwa hiyo hatuna uhusiano sisi kwa sisi,” ubaguzi mkubwa, “‘hatuna uhusiano wowote.’

101 “Basi sikilizeni kile Yeye alichosema, ‘Kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe. Nami ningekuletea maji, usije hapa kuteka.’

“Akasema, ‘Kisima ni kirefu, huna kitu cha kuchotea.’

102 “Basi walipokuwa wakiendelea na mazungumzo yao juu ya kuabudu mlimani, na kadhalika, ndipo tukamsikia Bwana wetu akisema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’

“Ndipo akageuka, na kusema, ‘Sina mume.’

103 “Ndipo tukawazia, ‘Ni kitu gani hiki? Je, Bwana wetu amekosea, wakati mwanamke huyu aliposema ya kwamba—ya kwamba hana mume? Mara nyingi kadiri ambavyo tumemwona akifanya ishara hiyo ya Masihi, halafu huyu hapa amesimama na tabaka jipya la watu, Wasamaria, na hata hivyo, hapa kwenye jambo la kwanza kabisa Yeye anashindwa!’

“Akasema, ‘Sina mume.’

104 “Kisha akasema, ‘Kweli. Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.’” Yeye hakosei.

“Ndipo akamwambia, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.’”

105 Yale mwanamke huyo aliyojua! Wakati siku chache tu hapo kabla, wakati alipofanya jambo lile lile, watu wa kanisa walimwita ibilisi, mwanamizimu, Beelzebuli, kasema, “‘Alikuwa akisoma mawazo ya watu, telepathia ya kiakili, ama kitu kama hicho.’” Kasema, “Yeye ni Beelzebuli akifanya jambo hili.”

106 Yesu akasema, ‘Mkisema hayo dhidi Yangu, nitawasamehe, lakini kwa njia nyingine, siku moja Roho Mtakatifu atakuja kunishuhudia, na wakati atakapokuja na kufanya jambo lile lile, kusema neno moja dhidi Yake hakutasamehewa katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.’” Hivyo ndivyo lingekuwa jambo baya.

107 “Naye akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.’” Sasa, msikilizeni mwanamke huyu. “‘Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Masihi yuaja, na Masihi ajapo, Yeye atafanya mambo haya, atatwambia mambo haya, hiyo itakuwa ndiyo ishara ya Masihi ajapo, kwa hiyo hapana shaka Wewe ni Nabii Wake.’”

108 Kwa maneno mengine alisema jambo lile lile walilosema hao wengine, “‘Masihi atakapokuja, Masihi atakuwa ni Nabii, Mungu-Nabii. Atakuwa zaidi ya Nabii, bali ataonyesha ishara

ya Masihi kama Nabii.” Hawakuwa na manabii kwa miaka mia nne na kitu, tangu Malaki, mmoja wa manabii wadogo.

109 “Kasema, ‘Lakini Masihi ajapo, Yeye atakuwa Nabii kama Musa, Nabii mkuu, ambaye atajua mambo kimbele, na kusema mambo, na kutwambia kile tulicho, yale tumefanya, atakuwa Mtu wa namna hiyo. Ninajua ajapo Masihi Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?’”

“Yesu akasema, ‘Mimi ninayesema nawe Ndiye.’”

110 Sasa, wakati mwingine nimesikia, kafiri mmoja akisema si muda mrefu uliopita, “Hakuna mahali hata pamoja katika Maandiko ambapo Yesu aliwahi kusema ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Kristo.” Vipi kuhusu hilo, na mahali pengine, pia?

111 Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

112 “Na juu ya hili akaangusha, akaweka chini, ama akaangusha mtungi wake wa maji, na kukimbia mjini, na kusema, ‘Njoni mwone Mtu ambaye ameniambia yale niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?’” Nayo Biblia ilisema ya kwamba mji huo ulimwamini Yeye kuwa ndiye Masihi kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo.

113 Sasa, kama hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi leo (Je, hiyo ni kweli?), kama Yeye ni yule yule.

114 Sasa hebu tusimame tu kwa muda kidogo. Sasa, kuna matabaka matatu ya watu duniani kama Biblia ni ya kweli. Na Mungu anisamehe kwa neno hilo la kukufuru la “kama.” Biblia *ni* ya kweli. Nasi sote tunatokana na watoto wa Hamu, Shemu, ama Yafethi, hao walikuwa ndio wale wana watatu wa Nuhu, baada ya mafuriko yaliyotangulia ile gharika wakati ulimwengu ulipoangamizwa tu—tunatoka kwa hao watu watatu, sasa, hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

115 Hivi mliona? Petro alipewa katika Mathayo, ninaamini mlango wa 16, funguo za Ufalme wa Mbinguni. Na kwenye Siku ya Pentekoste akaufungua kwa Wayahudi.

116 Filipo alishuka na kuwahubiria Wasamaria hawa, na hata hivyo Roho Mtakatifu hakuwa amemshukia hata mmoja wao, hata hivyo yeye alikuwa na Roho Mtakatifu. Waliagizia na Yohana na Petro wakashuka wakaja, wakawawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Sawa. Mnaona? Ingawa huyo mtu alijaa Roho Mtakatifu, hata hivyo Petro ndiye aliyekuwa na funguo. Basi hilo lilikuwa ni taifa lingine la watu, Wasamaria.

117 Halafu, nyumbani mwa Kornelio, wao... Kornelio alikuwa ameona ono nao, uh, yule Malaika alimwambia ashuke aende kwa Simoni mtengeneza ngozi, aulizie mtu mmoja, Simoni. Naye akaja na kumwambia mambo ya Bwana. “Basi Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia.”

¹¹⁸ Lakini mnaona tangu wakati huo na kuendelea, Paulo, yeyote wa hao wengine waliwawekea mikono, na kadhalika, wakampokea Roho Mtakatifu. Lakini kulikuwako na matabaka hayo matatu ya watu tena, watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi: Wayahudi, Wamataifa, na Wasamaria.

¹¹⁹ Sasa angalieni, Yesu alipokuja, Yeye alifanya ishara hiyo, kama ishara ya Masihi, mbele ya Wayahudi. Sasa, Wamataifa, sisi Waanglo-Sakson, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote; Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Yeye ataponya tu, usiku wa leo, wale wanaoamini wata—wataponywa, atawaokoa tu wale walio na imani ya kutosha kuokolewa, atawajaza tu kwa Roho wale wanaomtazamia Roho Mtakatifu. Atakapokuja duniani tena, atakuja kwa ajili ya wale wanaomngojea Yeye aje, na kumtazamia Yeye kuja, na wamejitayarisha kwa ajili ya kuja Kwake, Yeye atakuja kwenye Kanisa Lake.

¹²⁰ Sasa, sisi Waanglo-Sakson, Wamataifa, hatukuwa tukimtazamia Yeye kuja, bali kulikuwako na matabaka mawili yakimtazamia Yeye kuja, hayo yalikuwa ni Wayahudi na Wasamaria. Nanyi yachunguzeni Maandiko yote, wala kamwe hamtapata mahali pamoja ambapo Yesu aliwahi kufanya ishara hiyo ya Masihi kwa Mmataifa, si hata wakati mmoja, kwa sababu Mataifa hawakuwa wakimtazamia. Lakini Yeye alisema katika siku za mwisho Roho Mtakatifu atakapokuja atafanya hivyo.

¹²¹ Wa—Wamataifa hawakuwa wamefundishwa juu ya dini ya Yehova, hawakuwa wakitazamia kitu kama hicho, hawakufundishwa mafundisho ya Biblia. Tulikuwa makafiri walioabudu sanamu, Warumi, na Wayunani, na kadhalika, waliokuwa na miungu na miungu wa kike, tukibeba rungu mgongoni mwetu, na kadhalika, makafiri. Lakini Wayahudi na Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi, ndipo Masihi alipokuja, Yeye aliwaonyesha ishara ya Mungu-Nabii, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Masihi.

¹²² Sasa, Yeye alisema, “Katika kuja kwa siku za mwisho,” sasa sikilizeni kwa makini, Yeye alisema, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sasa, kabla tu ya hapo Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.” Sasa, angalieni, wakati wa Nuhu ilinyesha mvua, akasema, “Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa.” Huo ulikuwa ni utovu wa uadilifu, kwa sababu huko Sodoma walikuwa wamepita hayo. Mnaona? Yeye alisema, “Katika siku za Nuhu, kabla ya ile gharika, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa,” lakini basi ilipofikia siku za Sodoma, Yeye hakutaja jambo moja kuhusu hilo. Mnaona?

¹²³ Loo, Mungu amejaa hekima. Yesu alimshukuru Baba kwa sababu alikuwa ameyaficha kutoka kwa macho ya wenye hekima

na akili, huwezi kulipata kwa kulichambua. Mungu ni Ufunuo. Ilikuwa ni ufunuo hapo mwanzo. Ni nani aliyemwambia Habili, ya kwamba anapaswa kumtoa mwana-kondoo, badala ya Kaini pamoja na tunda?

¹²⁴ Wakati Yesu angeninii, aliwauliza wanafunzi Wake, “Watu hunena Mimi, Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

Na mmoja akasema, “Wewe ni Musa.” Ndipo mmoja akasema, “Wewe ni Eliya, ama manabii.”

Akasema, “Lakini ninyi mwasema ni nani?”

Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

¹²⁵ Akasema, “Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

¹²⁶ Ni ufunuo wa kiroho, kwamba Yesu Kristo ni Nani. “Juu ya Mwamba *huu*,” Mungu, akifunua, si kwa kujifunza kwa neno, si kwa kanuni fulani ya imani, bali kwa ufunuo wa kiroho, ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu ambaye amefunuliwa kwako na Roho Mtakatifu.

¹²⁷ Biblia ilisema, “Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu.” Hivyo ndivyo ilivyo muhimu siku hizi. Lakini tunaona ulimwengu umeingia wazimu wa anasa, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu.

¹²⁸ Angalieni Reno, Nevada, hapa nyuma, wakioa, wakiolewa. Angalieni sasa, kama siku za Nuhu, na siku za Sodoma, angalieni ule upotovu. Barua, maelfu yazo yakitoka, sana sana zikitoka California hapa, ambapo upotovu unaendelea, loo, jamani, unaenea haraka, ukiongezeka yapata asilimia thelathini kila mwaka, ya upotovu. Kwa sababu watu ni wa kawaida sana, na ni ninii sana. . . Loo, li—linachukiza sana!

¹²⁹ Hata si sawa kulizungumzia, hata kidogo, kutoka jukwaani, jinsi mataifa navyopotoka, na hasa sana Marekani hii, nchi yetu, makazi yetu. Loo, linahitaji mtikiso halisi, wa kweli, wa uamsho la sivyo litapata mtikiso wa atomiki. Kwa hiyo umepita uamsho, kwa hiyo tutangojea tu atomiki, bali Kanisa litaondoka kabla ya wakati huo kuja.

¹³⁰ Na kama hilo liko karibu hivyo na kuja kwa mitetemo ya atomiki, mpaka tunajenga mahali pa kukimbilia, cheche za mnururisho na vitu kama hivyo, vipi kuhusu Kuja kwa Bwana? wakati hilo litatukia kabla ulimwengu haujaangamizwa, tunajua hilo.

¹³¹ Angalieni, Nuhu alikuwa ndani ya safina kabla ya maji yoyote kuanguka, ilimbidi Lutu kutoka Sodoma kabla ya Moto wowote kushuka, kanisa litaondoka ulimwenguni kabla ya bomu la atomiki kulipuliwa, itabidi litoke.

¹³² Angalieni, sasa hebu na tuangalie yale Sodoma ilifanya, ndipo tutarudi moja kwa moja.

Mnasema, “Ndugu Branham, umeenda mbali sana na somo lako.”

¹³³ Vema, kama vile David alivyosema wakati mmoja, David duPlessis alisema, “Siwezi kuhubiri kwenye barabara kuu wakati wote, kwa sababu wengi wa watu ninaowahubiria hawaishi kwenye barabara kuu, inanibidi kushuka kwenye kijia, niwachukue baadhi yao, nirudi tena.” Kwa hiyo nimeondoka kwenye somo langu, ila nilitaka kuwachukua baadhi yao huko chini kwenye kijia sasa.

¹³⁴ Sasa angalieni, juu ya hili “Katika Sodoma, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” hebu na tusimame tu kwa dakika chache hapa sasa juu ya ushuhuda wa Filipo, na hebu twende Sodoma kwa muda kidogo tu.

¹³⁵ Angalieni, Sodoma...Daima kuna matabaka matatu ya watu ulimwenguni, hayo ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, hayo ndiyo matabaka matatu wanayotoa daima.

¹³⁶ Na sasa, huko Sodoma kulikuwako na Msodoma, mnajua dhambi yake ilikuwa ni nini, ilikuwa ni mbaya sana, kama tu ilivyo u—ulimwenguni siku hizi. Vema.

¹³⁷ Sasa, halafu Ibrahimu...Sasa, Lutu alikuwa huko chini Sodoma, Mkristo vuguvugu, Mkristo wa kawaida, kwa sababu ilisema, “Dhambi za Sodoma ziliitesa nafsi yake yenye haki.” Lakini alifanya machache kulihusu, akawaruhusu waingie kanisani mwake wamevalia vyovyote watakavyo, wanafanya watakavyo, kuvuta sigara, kunywa pombe, kucheza kamari, na kufanya chochote, mradi tu walikiri kwamba ni waaminio, mnaona, ilikuwa sawa, Mkristo vuguvugu tu, mshiriki vuguvugu wa kanisa.

¹³⁸ Halafu, tunaona ya kwamba huko nje, huko juu jangwani, kulikuwako na Ibrahimu aliyetengwa, aliyetwa atoke, Kanisa teule, lililochaguliwa kwa kujua tangu zamani, Mungu alikuwa amemwita atoke. Neno lenyewe *kanisa* linamaanisha, “walioitwa watoke na kutengwa.”

¹³⁹ Israeli walikuwa watu wa Mungu mpaka walipoitwa kutoka Misri na kutengwa na Wamisri, na kisha wakawa Kanisa la Mungu. Neno *kanisa* linamaanisha, “walioitwa watoke.”

¹⁴⁰ Hawa hapa, Ibrahimu ameketi kule juu, mambo yanakuwa magumu kwake. Ningewazia Bibi Lutu alitembea huku na huku kwenye maskini jumba lake la pembe za ndovu huko chini Gomora, na kusema, “Unajua nini? Kuna maskini, kizee Sara kule juu, karibu hata hana nguo za kubadilisha, huyo hapo Ibrahimu, mifugo yake ikifa kwa njaa. Kwa nini wasishuke waje hapa na kujiunga na mashirika yetu?”

¹⁴¹ Lakini ndugu, walikuwa na jamii moyoni mwao, walikuwa na kitu fulani mle...?...wakingojea kuja kwa Bwana. Siku moja wakati hali ya hewa ilikuwa joto kuliko ilivyo leo, kavu kama ilivyokuwa, Ibrahimu alikuwa ameketi mlangoni pa hema lake, ambapo walikuwa na mwaloni wa kale (Nami niliwazia hilo Ndugu Bud, kama uko hapa ndani, nilipokuja nyumbani kwako leo.), naye ameketi hapo karibu na hema, nao wachungaji walikuwa nje, na maji yalikuwa yamekauka kabisa, na ilikuwa vigumu kwao kupata chochote kwa ajili ya mifugo yao.

¹⁴² Basi muda si muda mwajua, ilitokea kwamba Ibrahimu aliona hawa hapa wanakuja watu watatu wamejaa mavumbi kote nguoni mwao, watu wa kawaida tu. Ibrahimu akawazia, mwajua, ya kwamba hapana shaka kuna jambo fulani tofauti kuhusu jamaa hao, aliwakaribisha ndani na kuwaketisha chini.

¹⁴³ Akasema, “Ketini. Hebu nilete maji kidogo, nikawaoshe miguu yenu, mjiburudishe, nami nitaleta chakula kidogo, mkale chakula, kisha mwende kokote mwendako.” Kwa sababu Ibrahimu aliamini ya kwamba kulikuwa na jambo fulani lililokaribia kutukia.

¹⁴⁴ Mwajua, kuna jambo fulani kuhusu wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Mwajua, hisi ile ile ya kutekenya-tekenya moyoni mwa Ibrahimu ya kwamba kuna jambo fulani linalokaribia kutukia ni kitu kile kile kilichomtuma mama huyu hapa usiku wa leo pamoja na hiki kiti cha magurudumu, kile kile kilichomtuma mtu yule *pale*, kile kile kilichomtuma kila mmoja wenu hapa. Hisia hiyo ndogo kwamba kuna *kitu fulani* mahali fulani, mnaona, umekuja tu kwa kusudi hilo, kwa sababu... .

¹⁴⁵ Loo, mtu fulani angesema, “Loo, hilo ni kundi la—la watakatifu wanaojibingirisha huko juu, ama chochote zaidi.” Mnaona, hawaelewi. Lakini Roho Mtakatifu aliwaongoza hapa. Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.

¹⁴⁶ Sasa, wakati hawa watu wawili, watatu walipokuja, wakaketi chini, basi Ibrahimu aliingia hima ndani, kasema, “Sara, chekecha unga kidogo.”

¹⁴⁷ Ni wangapi wamewahi kuchekecha unga? Jamani, baadhi yenu wanawake, hakika, wengi wa hawa, mmoja mwenye maskini nywele zenye mvi...Nimemwona mama yangu akichukua hilo chekecheo la kale namna hiyo, lililokuwa na kabari ndani yake. Wakati mwingine unga ungekuwa na mabonge, naye ingembidi kuchukua kabari hii na kuikwangua huku na huku na huku kutoa ninii, kuyatoa, na kuoka maskini hizo keki za mahindi kwa ajili ya kiamshakinywa, na kula hizo na molasi ya mtama. Hakika. Pia alikuwa na maskini hii... .

¹⁴⁸ Naye akauchekecha namna hiyo, mwajua. Kisha—kisha akakimbia kwenye mifugo na kuchukua maskini ndama aliyenona, akamchinja, na kumwandaa, kisha akachoma nyama

mekoni, halafu akatoka. Nao, hawa watu watatu walikuwa wameketi pale, akawapa chakula. Sasa, angalieni sasa, tumerudi moja kwa moja kwa Nathanaeli, kwa muda kidogo tu, na ushuhuda wao.

¹⁴⁹ Sasa, alipotoka na kuwapa nyama, wakati watu hawa wameketi pale na kula, huku Ibrahimu labda anazungumza nao, baada ya kitambo kidogo akaona Mmoja wao aliendelea kuangalia upande wa Sodoma, wawili wao wakaamka wakaenda zao Sodoma.

¹⁵⁰ Na kwa hiyo, baada ya wao kushuka kwenda Sodoma... Mnakumbuka ujumbe wao ulikuwa nini walipofika kule chini? Toba! "Tokeni!" Huyu alikuwa ni Billy Graham mamboleo, na Oral Roberts, ama chochote unachotaka kuuita, wahudumu wawili mashuhuri, wenye nguvu walioshuka kwenda huko Sodoma na kuhubiri toba. Hawakufanya miujiza mingi, walipofusha tu macho machache. Nako kuhubiri Injili humpofusha asiyeamini.

¹⁵¹ Kwa hiyo yeye... Wa—wao hawakufanya mwujiza kama huo, walifanya miujiza, bali si miujiza kama iliyokuwa huko nyuma mahali pale pengine. Sasa, walihubiri, na kuwahimiza, "Tubuni la sivyo mtaangamia." Hao walikuwa wale wawili walioshuka kwenda Sodoma.

¹⁵² Lakini Yule aliyebaki hapa nyuma pamoja na Ibrahimu, hebu tumwangelie kwa dakika chache. Kanisa, toleo la mwaka wa mia tano na kitu A.D. la Pentekoste, ameketi pale chini hemani, mwaminio. Ndipo Mtu huyu alikuwa ameelekeza mgongo wake kwenye hema. Wanawake wakati huo hawakuwa kama wanawake siku hizi, sana sana, mnajua, ambao inawabidi kuwa katika shughuli zote za mwanaume na kadhalika, kwa namna fulani walikaa nyumbani, kwa hiyo wao—wao— kwa hiyo wao... Alikuwa, Sara alikuwa... Kamwe hujui.

¹⁵³ Kwa hiyo Mtu huyu, baada ya Yeye kumaliza kula, Yeye alisema, "Ibrahimu," angalieni, akamwita kwa jina, "Ibrahimu, yu wapi mkeo?" Alijuaje alikuwa ameo? "Yu wapi Sara, mkeo?" Sikilizeni hilo, kwa kweli jina lake halikuwa Sara, Sarai, kwanza, kisha akaitwa Sara, kwa sababu alikuwa binti mfalme, Yeye alimwita kwa jina lake la kifalme.

¹⁵⁴ "Ibrahimu, hilo ndilo jina lako, yu wapi mkeo? Kwa kuwa wewe ni mwanamume aliyeoa, na jina lake ni Sara." Alijuaje hilo?

¹⁵⁵ Angalieni hiyo ishara, sasa kumbukeni, Yeye alisema, "Kama tu ilivyokuwa huko Sodoma," wakati Moto ulipoiteketiza dunia, Sodoma na Gomora, "ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Sasa angalieni, ishara iyo hiyo, ilitolewa kwa ulimwengu wa Mataifa. Mnaona kile tunachofikia?

"Yu wapi mkeo, Sara?"

156 Ibrahimu akasema, “Yuko hemani.” Nayo Biblia ilisema hilo hema lilikuwa nyuma ya huyo Malaika. Ni wangapi waliowahi kusoma hilo, wanaojua hiyo ni kweli? Hakika. Hilo hema lilikuwa nyuma Yake. “Yuko hemani nyuma Yako.”

157 Kasema, “Ibrahimu, miaka ishirini na mitano iliyopita,” kwa maneno mengine, “Nilikuahidi mwana. Nitakuzuru kwenye muhula wa Sara,” zile siku ishirini na nane, kasema, “Ni—nitakuzuru kwa muhula huo, nawe utampata huyo mwana.”

158 Naye Sara, akiwa na umri wa miaka tisini, naye Ibrahimu mia moja, akafanya, “*Huf!*” nafsini mwake, akachekeka, akatabasamu kimoyomoyo nyuma ya Malaika, ndani ya hema.

Ndipo yule Malaika akasema, “Kwa nini Sara akachekeka?” Amina. Sasa, hiyo ilikuwa ni telepathia ya namna gani?

159 “Ibrahimu, wewe ni mtu aliyeoa, una mke, jina lake ni Sara. Sijawahi kukuona hapo kabla, kamwe sikujua lolote kukuhusu,” kwa maneno mengine, “hujawahi kuniona Mimi hapo kabla, bali unajua ya kwamba kuna jambo fulani linaloendelea.”

Sasa, “Yu wapi mkeo, Sara?”

Ibrahimu akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Naye akafanya, “*Huf!*”

160 Akasema, “Kwa nini akachekeka?” Hemani nyuma Yake! Hiyo ilikuwa ni kwa Kanisa teule. Sodoma haikuliona kamwe, Sodoma haikulijali. Lakini Ibrahimu alingojea katika hema lenye joto, lenye joto kuliko jengo hili alasiri ya leo, akingojea jambo fulani litukie, naye akalipata.

161 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kanisa lililoteuliwa litaona ishara iyo hiyo tena.

162 Sisi ni nini? Mnaona, Mataifa, yakimngojea Masihi. Mungu ni mwenyezi. Kama Mungu akiruhusu... Katika wakati wa mafundisho yote ya kiakili ambayo Israeli walikuwa nayo, na Samaria walikuwa nayo, na mwishoni tu mwa mafundisho yao, mwisho wa siku yao, Yeye aliwaonyesha ishara ya Masihi kuthibitisha jambo hilo ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hataruhusu Kanisa la Mataifa liingie bila kuwafanyia jambo lile lile.

163 Kama ingalikuwa hivyo, Yeye aliwapa kitu ambacho asingetupa sisi. Alimpa mmoja wa watoto Wake kipande cha sambusa, na huyo mwingine kipande cha sambusa, lakini akamkataza huyo mwingine. Hiyo... Yeye si Baba wa namna hiyo. La. Atawapa, kama wako tayari kuila. Jambo ndilo hilo. Ni juu ya Kanisa basi, ni juu yao.

164 Sasa, kama Filipo alivyoketi pale, na kusema, “Naam, hiyo ni kweli. Ndipo tulipoenda na kumwita Nathanaeli, naye Nathanaeli akasema hivyo, ama, Andrea. Wote wameshuhudia.”

Kasema, “Naam, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, jinsi ambavyo tunajua mambo hayo ambayo—ambayo Yeye alisema yangetukia.”

¹⁶⁵ Sasa, akasema, “Naam, moyo wangu uliwaka ndani yangu. Nikaanguka kifudufudi, ndipo wakati Yeye aliponiambia mahali nilipokuwa na kuniambia baba yangu alikuwa ni nani, basi wakati sote tuliposimama pale na kumwona mwanamke yule Msamaria, Naye akanwambia ya kwamba alikuwa na waume watano, na—na halafu kumwambia ninii . . . Akasema hakuwa na mume, Naye akasema, ‘Una watano, na yule unayeishi naye sasa siye wako.’

¹⁶⁶ “Basi alilia, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ajapo Masihi Yeye atatuambia mambo haya yote, lakini Wewe ni Nani?’” Mnaona? Sasa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁶⁷ Mnaomba usiku kucha, na kufanya mikutano hiyo midogo, mnasimama pembeni, mnapiga tari, nao polisi wanawasukumia kwenye kona moja, mnarukia kona ya kichochoro na kuanza tena. Mnaona?

¹⁶⁸ Hao walikuwa wakijaribu kuueneza ujumbe. Lakini tumefikia mahali sasa hata wahubiri wetu ni wa kiakili, na loo, wao ni Madaktari wa Uungu, na watu mashuhuri, wakubwa, na kadhalika. Hilo ni baya sana kwamba lilitukia, bali li—li—lilitukia, kwa vyovyote vile. Mnaona? Nasi hatuko kichochoroni tena, tuko moja kwa moja hapa nje kama makanisa mengine, majengo makubwa. Na mmoja anajaribu kumshinda mwenzake, kupata wengi zaidi katika shule yake ya Jumapili kuliko huyo mwingine, kila kitu namna hiyo.

¹⁶⁹ Nawe unajua nini? Nafikiri kwa jumla, tumeenda kombo bila Bwana. Mnaona? Mungu anapendezwa na sisi kuwaokoa watu, si kujenga majengo, ambayo majengo ni sawa, bali anataka watu waokolewe. Yesu kamwe hakuwaagiza wanafunzi Wake kujenga kanisa, kamwe hakuwaagiza kujenga hospitali. Mambo hayo yote ni sawa, bali Yeye alisema, “Hubirini Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

¹⁷⁰ Lakini tumeingia kwenye ishara za kiakili, wajukuu. Lakini Mungu hana wajukuu, mwajua, Mungu ana wana na binti pekee, si wajukuu. Mungu . . . Lakini tuna wajukuu wa Kipentekoste, kwa sababu baba na mama walikuwa wafuasi wa kanisa la Kipentekoste, tunaingia—tunaingia pamoja nao, walituingiza ndani, wakatuweka kwenye kitanda cha watoto, nasi tukawa washiriki wa kanisa la Kipentekoste. Hao ni wajukuu, hilo si zuri.

¹⁷¹ Tuna . . . Kila mtu amjiaye Mungu hana budi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, ndipo ninyi ni wana na binti za Mungu, wenye ujuzi, kitu fulani mle ndani ambamo Mungu anaishi, nawe unajua Yeye ni halisi. Huyu ndiye mwana na binti halisi.

172 Iwapo wewe—iwapo wewe ni Mmethodisti na ni mwana wa Mungu, amina, wewe ni Mwana wa Mungu Mmethodisti. Kama wewe ni Mpentekoste na ni mwana wa Mungu, vema, bali usiwe *mjukuu* Mmethodisti ama *mjukuu* Mpentekoste, kuwa mwana au binti kwa kuzaliwa, kuzaliwa upya, wa kimbinguni, ubatizo wa Roho Mtakatifu moyoni mwako, ndipo ninyi ni wana na binti.

173 Sasa, wanaona... Shetani aliangalia, naye akawakuta wakienda kwa hamaki namna hiyo, akasema, “Hii ndiyo nafasi yangu!” Kwa hiyo akainua kichwa chake kinachoteleza juu ya kilima, na kuanza kuvuma ziwani mwajua, “*Whiu! Whiu!*” Upepo ukaja, pepo za sumu zikaanza kuinuka juu chini ya bahari na kukisukasukuka maskini chombo hicho.

174 Nanyi, mwajua, wakati ubaridi huo unapoingia, nasi tunaanza kuwazia juu ya wahudumu wasomi, “Vema, mchungaji wangu ana D.D. Mchungaji wangu ana di—digrii ya Shahada ya Sanaa. Mchungaji wetu anatoka katika seminari *Fulani-fulani*,” hilo halimaanishi chochote, hata kidogo. Afadhali mtoto wangu angekuwa na mtu ambaye hata hakujua ABC zake, naye ana Kristo moyoni mwake, kuliko kuwa pamoja na mtu aliyejua mambo yote ya kiakili. Hiyo ni kweli.

175 Musa alijua mambo yote ya kiakili, lakini ilimbidi Mungu kumpeleka kichakani na kumwondolea yote, na kisha kuweka imani fulani ndani yake kutoka kwenye Moto uliokuwa kwenye kile kichaka. Na hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo ni ziara nyingine ya kichakani, ambapo tunapata tukio.

176 Leo hii tunaishi katika siku ambapo makafiri wanajaribu kuelezea yote vinginevyo. Yesu alijua hayo, akasema, “Sitawaacha yatima, Baba atamtuma Roho Mtakatifu katika Jina Langu. Na baada ya kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” Roho Mtakatifu akinena ndani Yake, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.”

177 Sasa, Mungu alijua ya kwamba katika mwisho wa ulimwengu watu wangeinuka, wasomi mashuhuri na wenye elimu, na kuelezea Biblia yote vinginevyo. Wala hakuna mtu aliye na haki nyuma ya mimbara, hakuna mtu aliye na haki ya kujiita Mkristo, mpaka wakati mmoja amerudi kule upande wa nyuma ya jangwa chini ya mchanga huo mtakatifu ambapo alikutana na Mungu uso kwa uso, alikuwa na tukio.

178 Huenda ukawachukua Madaktari wote werevu, wa Uungu kuelezea *hili* vinginevyo, na kueleza *hayo* yote vinginevyo, lakini inapofikia kukanyaga mchanga huo mtakatifu ambapo ulikutana na Mungu uso kwa uso, hakuna Madaktari wa Uungu wa kutosha, ama hakuna pepo wa kutosha kutoka kuzimu wangeweza kamwe kulitikisa tukio hilo kutoka kwako.

179 Wakati umekutana na Mungu mahali fulani uso kwa uso, na kuhisi nguvu za badiliko la maisha mapya zikija ndani yako,

hakuna ibilisi katika kuzimu angaliweza kamwe kuuondoa kwako, wewe ni kiumbe kipya, nawe unao huo ujuzi moyoni mwako, unasema, “Lakini ngoja kidogo, ngoja kidogo! *Jambo fulani* lilitukia.” Unaona? Una *kitu fulani*.

¹⁸⁰ Ninakumbuka wakati mwangalizi mkuu alipokuja, naye akasema, “Billy, hapana shaka ulipatwa na jinamizi.”

Nikasema, “Kama ndivyo ilivyo, hii *hapa* kadi yangu ya ushirika. Nilikutana na Mtu aliyesema nami, ilikuwa ni Uzima kwangu.”

Nikasema, “Hii hapa . . .”

“Loo,” akasema, “usijisikie hivyo kulihusu.”

¹⁸¹ Nikasema, “Vema hiyo ni hisia yangu tu, kwa vyovyote vile. Siwezi kufungwa kabisa hapa, na kumtumikia Mungu, nitamtumikia tu moja kwa moja, mimi na Yeye tu pamoja.”

¹⁸² Sasa, angalieni tunapofunga, pepo zinaanza kuvuma, pepo za sumu. Kumekuwako na pepo nyingi sana zimekuwa zikivuma leo, zikisema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili ya wakati mwingine, miaka elfu mbili iliyopita.”

¹⁸³ Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Huo ndio umbali linaoenda, hilo ni kadiri tu lingeweza kwenda, lakini, mnaona, wana kitu fulani wanachotaka kufananisha ulimwengu ndani yake; tutaingilia hilo baadaye.

¹⁸⁴ Ndipo basi pepo zikaanza kuvuma, na matumaini yote ya uamsho yalikuwa yamekwisha, kila kitu kilikuwa kimetoweka kabisa. Ile meli ndogo ilininii. . . ilijaa maji, makasia yalikuwa yamevunjika, nao hawa hapa wakirushwarushwa, na kupigapigwa, wakiyumbishwa huko nje juu ya mawimbi kama kizibo cha chupa kwenye ba—bahari yenye nguvu. Nao hao hapo, hawana matumaini kabisa ya kufika ufukoni, nao wote wangekata tamaa.

¹⁸⁵ Lakini mnajua nini? Hakuwa amewaacha, bila shaka hakuwaacha. Alipanda kilima kirefu sana ambacho angeweza kupanda, ili aweze kuangalia kote upande wa pili wa bahari, Naye aliwaona walipokuwa katika shida. Naye huyu hapa anakuja akiwaendea juu ya maji.

¹⁸⁶ Ndugu, Yeye alitufanyia jambo lile lile, Yeye hakupanda tu kilima kilicho kirefu zaidi, alipanda kilima pale Kalvari, alienda kwenye Mlima Kalvari na kupandia hapo vile vipandio vya dhahabu, mpaka akaingia moja kwa moja katika Umilele, na kuketi mkono wa kuume wa Mungu, anaweza kuona mwi—mwisho tangu mwanzo. “Jicho Lake liko juu ya shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia.” Anakuangalia, Yeye anaangalia maskini mkutano huu, “Walipo wawili watatu

wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao.” Yeye anajaribu kupata mahali pa kujidhihirisha Mwenyewe, kufanya jambo kubwa, kufanya jambo la kuwasaidia, kuwaonyesha ya kwamba Yeye yupo hapa. Hajafa, Yu hai tena.

¹⁸⁷ Kila dini. . . Niliposimama pale alasiri hiyo mbele ya dini kumi na saba mbalimbali, nilisema, “Waungwana, kila mmoja wa waanzilishi wenu amekufa, na yuko kaburini, Buddha, Muhammad, na hao wengine wote, Makalasinga na Wajaini na hao wote, waanzilishi wenu wamekufa, na wamezikwa kwa mamia ya miaka, lakini Mungu wetu hajafa.”

Wakasema, “Vema, walimsulubisha.”

Nikasema, “Lakini Yeye alifufuka tena.” Nikasema, “Kama atajithibitisha Mwenyewe kuwa yu hai, mtampokea?”

“Naam, kama unaweza kutuonyesha yu hai.”

¹⁸⁸ Na ni, loo, sijui ni elfu ngapi waliompokea walipoona kwamba alikuwa hai.

¹⁸⁹ Maskini ile makala ya Bw. Graham si muda mrefu uliopita, wakati gazeti liliifuatilia, kasema, wao walisema, Bw. Graham alikwepa wala asingewaombea wagonjwa huko nyuma kwa huyu Mwislamu wakati alipompa changamoto, na kusema, “Sasa, vipi, vipi kuhusu Durban, Afrika Kusini,” kasema, “wakati William Branham alipokuwa kule, wakati Waislamu elfu kumi walipoanguka madhabahuni wakati mmoja?”

¹⁹⁰ Walipomwona mtu aliyekuwa ameteseka sana, alikuwa kwa kila njia, akamwambia yeye alikuwa ni nani, na mahali alipotoka, na yote kulihusu, na kumponya, akamwinua tu kwa miguu yake katika dakika moja, hata wakati akiwa hana akili timamu, akarudia akili yake ya kawaida, na machozi makubwa yakitiririka kwenye tumbo lake jeusi, na hapo akaponywa. Niliona Waislamu elfu kumi kwa wakati mmoja, na kwa jumla wasioamini elfu thelathini wakianguka msalabani.

¹⁹¹ Sio kujenga makanisa, bali kuhubiri Injili, hilo ndilo agizo, jambo ndilo hilo. Makanisa ni mazuri, shule ni nzuri, madaktari wote wako sawa, hospitali ni. . . Sikosoi hilo, lakini hayo siyo Ujumbe wa Kanisa, ni “Ithubirini Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio,” ilisema Marko 16. Haya basi.

¹⁹² Sasa, wakati jambo hili lilipotukia, mawimbi yalianza, huku na huku, na jambo la kuhuzunisha lilikuwa, zaidi sana ni kama ilivyo siku hizi, walipomwona akija, akitembea juu ya maji, walidhani ilikuwa ni kivuli, walidhani kilikuwa ni mzuka wa namna fulani, nao wakaogopa. Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia!

¹⁹³ Basi, marafiki zangu wapendwa, kama hiyo siyo hali ya siku hizi, sijui. Kitu pekee kinachoweza kuwasaidia watu, wanakiogopa. Wanasema, “Vema, hilo ni kundi la. . . Hilo huenda likawa ni watakatifu wanaojifingirisha. Huenda hilo

likawa ni kundi la Kipentekoste la lugha. Huenda ikawa, mwajua, huenda ikawa ni uabudu-mizimu. Huenda ikawa ni ibilisi.” Mnaona? Wanaogopa kitu cha pekee kinachoweza kuwasaidia.

¹⁹⁴ Huyo hapo anakuja akitembea. Na—nao wakaona ilikuwa... Ilionekana kama Yeye, lakini, loo, walilia kwa hofu, walidhani ilikuwa ni roho ya namna fulani.

Akasema, “Msiogope; Ni Mimi; Ni Mimi.”

¹⁹⁵ Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele basi atafanya vivyo hivyo leo kama alivyofanya wakati huo, na atafanya hivyo milele. Hiyo ni kweli?

Na tuinamishe vichwa vyetu tunapotafakari juu ya Maandiko haya.

¹⁹⁶ Baba yetu wa Mbinguni, tunapokaribia mwisho wa ujumbe huu mdogo, ulioparaganyika, nikitumaini ya kwamba Roho Mtakatifu atayachukua maneno hayo, na—na ayasambazie tu katika kila moyo kadiri walivyo na haja, jalia yazame ndani kabisa.

¹⁹⁷ Basi watu hawa wameketi hapa chini ya paa hili lenye joto, sio tu wapate kuonekana, bali wamekuja kwa sababu wanaona njaa na kiu. Sasa, Baba, ninakuomba ya kwamba Wewe utawahudumia baraka wanazozijia. Jalia kusiwe hata na mmoja atakayebaki akiwa mgonjwa au anayeteseka. Jalia kusiwe na yeyote hapa aliye na shaka lolote, jalia Roho Mtakatifu, pamoja na Neno la Mungu hapa, aondoe kila shaka niani mwao, kwa sababu, Baba, tumelitoa jinsi hasa lilivyoandikwa, Huyo *alikuwa* ni Masihi, hiyo *ilikuwa* ni ishara Yake, Huyo Ndiye *aliyeahidi* kwamba angekuwa.

¹⁹⁸ Sasa, Baba, tunamtazamia kufanya jambo lile lile usiku wa leo kama alivyofanya akija... wale waliokuwa Emau, alitembea pamoja nao siku nzima, aliwapenda, na kuzungumza nao, na kuwapa Maandiko.

¹⁹⁹ Kuna wengi wanaoketi hapa usiku wa leo, asilimia tisini ya kusanyiko hili waliinua mkono wao, kwa mara ya kwanza. Wanajua kumekuwa na Mtu fulani ambaye amewasaidia. Nilipowauliza tena, waliinua mkono wao, walikuwa ni waaminio Wakristo, waliliamini.

²⁰⁰ Sasa, wakati Kleopa na rafiki yake, wakitembea kutoka Emau, wakizungumza na Yesu, bila kujua Yeye alikuwa ni Nani, alipowaingiza ndani usiku huo na kufunga mlango, alifanya jambo fulani kama tu alivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, ndipo wakajua ya kwamba hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo kama Yeye, ndipo wakajua ya kwamba Huyo alikuwa Yesu wao yule yule, kwa sababu alifanya vile vile *baada* ya kufufuka Kwake kama alivyofanya *kabla* ya kufufuka Kwake,

nao wakatambua ya kwamba ilikuwa ni Yeye. Upesi akatoweka, mara alipofanya huo mwujiza, asionekane.

²⁰¹ Lakini walienda mbio, na kumwambia kila mtu, “Hakika Bwana amefufuka.” Ndipo wakakutana na wengine ambao tayari walikuwa wamehusishwa na ufufuo, wa kumwona baada ya kufufuka.

²⁰² Ninakuomba Wewe, Baba, ya kwamba wakati watu hawa wapendwa wanapovuka vilima hivi, wakishuka kwenda kwenye miji mbalimbali, na makazini mwao, jalia wazungumze usiku wa leo. Pia nijalie mimi, ninapoenda zangu kambini mwangu, jalia niweze kusema pamoja na wale walio pamoja nami, kama siku zile, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?”

²⁰³ Njoo usiku wa leo, Bwana Yesu, tunakaribia mwisho wa wakati. Jimbo hili kuu la California, sehemu kubwa ya wakazi wa Marekani inatoka hapa, mitindo inasambazwa kutoka hapa. Ee Bwana, huku juu kabisa katika watu hawa huku juu ziwani, wengi wao huko chini Los Angeles na mahali mbalimbali, jalia Roho Mtakatifu Wako aje mara nyingine tena, Baba, ili waweze kujua ya kwamba hiyo ndiyo ishara ya kwamba Masihi anakaribia. Ni kama tu lile—lile jiwe la pembeni, kama tu lile jiwe la kufunika juu ya piramidi, halina budi kushikana nayo, hayo mawe mengine hayana budi kushikana nayo, la sivyo kamwe haiwezi kufunikwa.

²⁰⁴ Ndivyo ilivyo na Kuja kwa Bwana Yesu, Kanisa halina budi kuchongwa *sana*, hata Kristo na Kanisa Lake watakuwa Mmoja, watakapokuja, kwa hiyo jalia Roho Wake atawale sana usiku wa leo mioyoni mwetu na katika mkutano wetu, hata kila mtu atatambua ya kwamba ni Wewe wala hawataogopa, watajua ni Wewe kwa sababu Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Haya tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁰⁵ Sasa, tutafanyiza mstari mdogo wa maombi. Tunaninii... Nimeona karibu kila mtu hapa walikuwa ni Wakristo. Nasi tutakuwa na miito ya madhabahuni tunapoendelea, kwa sababu uponyaji wa Kiungu si jambo kuu, uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo. Lakini asilimia themanini na sita ya huduma ya Bwana wetu Yesu ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu, hiyo ilikuwa ni kuwathibitishia watu kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

²⁰⁶ Sasa, ni wangapi watakaokubali ya kwamba yale niliyohubiri usiku wa leo ni Maandiko, hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe? Na ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye aliahidi kwamba katika siku hii ya mwisho angefanya, Yeye angerudi tena, afanye jambo lile lile katika siku za mwisho, ambalo alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya?”

²⁰⁷ Na ni wangapi wanaoamini katika kujua kwa Mungu tangu zamani? Kwamba Yeye, kutangulia kujua kisha akateua...

Uteuzi ni kwa kujua tangu zamani. Na halafu Mungu katika zile nyakati, alikuwa na Martin Luther, alikuwa na John Wesley, amekuwa na watu kote katika wakati, katika siku ya mwisho hana budi kuinua kitu fulani, Kanisa, ambalo huduma Yake itakuwa. . . Martin Luther, kuhesabiwa haki kulikuwa kwa imani, John Wesley alikuwa na utakaso, kazi ya pili ya neema, Pentekoste imekuwa na kurudishwa kwa karama, sasa, jambo linalofuata ni Kuja kwa Bwana.

208 Kwa hiyo, ujumbe huu wa karama ya kunena kwa lugha, kufasiri lugha, na mambo mbalimbali ambayo tumekuwa nayo, sasa unaingia moja kwa moja ndani, mpaka sasa umefikia saa ya Kanisa katika uchache, maana wanashuka kutoka kwa Wesley, Luther, na kuendelea moja kwa moja, sasa wamefikia kwenye kilele cha lile jiwe.

209 Sasa, amini kwa moyo wako wote. Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alisema jambo hili, ya kwamba “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, Yeye atazifanya, pia”? Hiyo ni kweli. Alisema hivi: “Bado kitambo kidogo na ulimwengu,” huo ni utaratibu wa ulimwengu, “hautaniona tena,” huyo ni asiyeamini, “hataniona tena, bali ninyi mtaniona,” huyo ni mwaminio, “kwa kuwa Mimi,” na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.” Ni wangapi wanaojua Yeye alisema hivyo?

210 Sasa, hilo linamfanya Yeye. . . Basi kama Yeye yupo hapa, kama Yesu amefufuka katika wafu, Naye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, Yeye ni kila kitu alichokuwa mbali na mwili wa kawaida. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba mwili Wake wa kawaida unaketi mkono wa kume na Mungu Baba Utukufuni, ukifanya maombezi? Kwa vile Mungu hawezi kuona dhambi zetu, Naye huangalia kupitia Damu ya Yesu, nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe, tunajua hilo, basi kupitia kwa Damu nyekundu ya Kristo, dhambi zetu nyekundu, zinageuka nyeupe. “Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji.”

211 Naye ameketi pale, usiku wa leo, kama Kuhani Mkuu, akituombea tunapokiri. Mnaamini hilo? Waebrania ilisema. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni, sasa hivi, kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Vema.

212 Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa, basi ungejuaje ulimgusa, kama Yeye hakutenda kama alivyotenda alipokuwa hapa duniani? Kama Yeye—kama Yeye si yeye yule. . . Huenda ukasema, “Vema, haleluya, nilimgusa.” Huenda ikawa hivyo, bali kama Yeye angali ni Kuhani Mkuu yeye yule, hana budi kutenda vivyo hivyo. Alitendaje wakati alipoguswa hapa duniani?

213 Maskini mwanamke mmoja, wakati mmoja Yeye alipokuwa akienda zake kumfufua maskini msichana mdogo, aliyekufa . . .

214 Naye Yesu alisema, “Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe kwanza.” Ni wangapi wanaojua hilo? Yohana Mtakatifu 5:19, alipitia karibu na birika la Bethesda, ambapo makutano, maelfu ya walemavu, viwete, vipofu, na waliopooza, akapenya kwenye umati huo mpaka akamwona mtu amelala kwenye godoro, kitu kama yule jamaa mdogo aliyelala pale, kwenye godoro, ndipo akasema . . . Yeye akamponya mtu huyo, kwa sababu Biblia ilisema kwamba Yesu alijua ya kwamba alikuwa hivyo miaka thelathini na minane.

215 Sasa, hakuwa kipofu, wala hakuwa kiwete, hakuwa ameshindwa kutembea, alisema, “Ninaposhuka, mtu mwingine hushuka mbele yangu.” Mnaona, angeweza—angeweza kupata . . . angeweza kutembea, hakuwa kipofu, si kiwete, wala hakuwa na—na kichwa kilichojawa maji, wala chochote kile alikuwa na ugonjwa uliodumaa, kitu kama TB, au ugonjwa wa tezi dume, ama chochote kile. Yeye. . . Ulikuwa umedumaa, alikuwa nao miaka thelathini na minane, haungemwua. Lakini Yesu alikuwa ameonyeshwa na Baba kwenda kule, Naye akaenda.

216 Vivyo hivyo na Samaria, alikuwa na haja kupitia Samaria, hakujua alilokuwa anaenda kufanya. Alipofika kule aliwatuma waende, na kuwazia, “Baba, ni kitu gani?” Ngojewa hapo, muda si muda mwajua, huyu hapa mwanamke huyu anakuja. Akaanza kuzungumza naye mpaka akashika roho yake, na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini. Sasa, huyo alikuwa ni Yesu jana.

217 Sasa, jambo pekee nijualo, nilipaswa kwenda Ujerumani, na kote Ulaya, niingie Asia, kote ulimwenguni, niizunguke dunia moja kwa moja huko Australia na New Zealand, nirudi. Jambo fulani likatukia, nisingeweza kwenda, kwa amri ya serikali ya Marekani, nisingeweza kuondoka. Vema. Sasa, nilifanya nini? Nikasema, “Ndugu Borders, nenda huko ukaandae mikutano kadhaa.”

Muda si muda mnajua akasema, “Vema, ninayo *hapa*, na *hapa* chini, na *hapa* chini.”

Nikasema, “Ni sawa kwangu, sina uongozi dhahiri.”

218 Lakini Baba akaniongoza hapa, mimi hapa. Sikujui, kuwa wewe ni nani. Sasa, Yeye atafanya nini? Ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, atatenda vile vile jana, leo, na hata milele kama Yeye alinituma huku. Hiyo ni kweli? Alimwendea tu mmoja kule, lakini huyo alienda kwenye mji mzima na kuufanya huo mji mzima uamini. Mnaona?

219 Sasa, mwanamke huyu, akienda Zake kumfufua binti Yairo aliyekuwa amekufa, sasa, wakati alipokuwa njiani kule juu, maskini mwanamke mmoja, asingeweza kupata kadi ya maombi

na kuingia mstarini, tuseme. Asingeweza kumfikia, kwa sababu wengi sana walikuwa karibu Naye.

220 “Halo, Rabi, Wewe ndiwe Nabii wa Galilaya? Loo, unataka kuniambia . . . ? Je, utafanya mwujiza wakati ukiwa hapa pamoja nasi? Utakaa hapa ndani kwa muda gani?” Na kadhalika namna hiyo.

221 Lakini maskini mwanamke huyu alikuwa na kutokwa na damu kwa miaka mingi, naye akasema, “Yeye ni Mtu wa Mungu. Kama nikiweza kugusa upindo wa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Mnakumbuka hadithi hiyo? Naye akatambaa chini kupitia kwao na kujipenyeza humo, alikuwa anakaribia zaidi kidogo. Labda mtu fulani akamsukuma nyuma, kisha baada ya kitambo kidogo akakaribia vya kutosha, akaligusa vazi Lake. Sasa, vazi la Kipalestina linapwaya, likiwa na vazi la ndani. Hakuhisi mguso namna hiyo. Kwa hiyo, ililithibitisha hilo kwa dakika moja tu.

222 Naye akaligusa vazi Lake, akarudi mbio na kuketi chini, kama ulivyo wewe, ama chochote kile. Huenda alisimama, sijui, lakini hata iweje, Yesu alisimama, na kusema, “Ni nani aliyenigusa? Ni nani aliyenigusa?”

223 Mbona, Petro alimkemea, kwa maneno mengine yeye alisema, “Unasema nini? Ati ‘Ni nani aliyenigusa?’ Mbona, U—U—Unaongea kama mtu asiyejua walichokuwa wanazungumzia! Vema, kila mtu anakugusa.”

224 Akasema, “Naam, lakini huu ulikuwa mguso wa namna nyingine.” Huo ndio mguso tunaotaka. Mnaona? Tunataka wa aina hiyo. Kasema, “Mtu fulani alinigusa, kwa sababu nimekuwa dhaifu.” Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Mbona, ilisema nguvu zilimtoka, na nguvu ni uweza. Kasema, “Nimekuwa dhaifu.”

225 Ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko hilo mpaka akamwona maskini mwanamke huyo, na kumwambia alisema alikuwa anatokwa na damu, na kusema, “Imani yako imekuokoa.” Hiyo ni kweli?

226 Akamgusa, na ikamfanya ageuke na kuongea naye. Sasa, kama Yeye ni yule yule usiku wa leo, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, iwapo utaamini tu kwa moyo wako wote na kumgusa Yeye kwa imani yako, ondoeni tu kutokuamini kwote, na madhehebu, na mashirika, na yale *Fulani-wa-fulani* aliyosema juu yake, achaneni tu na hayo yote, na kusema, “La, ninaamini Yeye ni Mwana wa Mungu, mimi—mimi ni mgonjwa, ninamhitaji,” na—na ninaweza tu kumgusa, basi jambo fulani litatukia kwako, kama tu ilivyotukia kule, kama utaamini. Utafanya hivyo kama Yeye atalifanya?

227 Sasa, hebu . . . Nafikiri Billy alisema aligawa karibu kadi hamsini ama mia moja za maombi.

228 Hebu . . . Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Hebu tuanzie kwenye namba moja, yapata . . . kama tukienda kwa upambanuzi tutaninii . . . Shikilia tu kadi yako nisipokufikia usiku wa leo.

229 Lakini hebu tu—hebu tulete baadhi hapa juu ili tuone kile Roho Mtakatifu atakachofanya, kwa ajili ya watu walio hapa kwanza.

230 Kadi ya maombi namba moja. Loo, samahani! Yeye alinirii . . . Amegawa kuanzia hamsini, hamsini hadi mia moja? Nilifikiri alisema moja hadi mia moja.

231 Vema, ni nani aliye na kadi ya maombi namba hamsini basi? Inua mkono wako. Namba hamsini. Vema. Hamsini, hamsini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano, -sita, -saba, -nane, -tisa, sitini, hamsini hadi sitini, wasimame, na sitini hadi sitini na tano. Vema. Hebu wasimame, waje huku, kama mnaweza kusimama. Kama huwezi kusimama basi mabawabu watakuchukua na kukuleta hapa, ama uinue tu mkono wako, nasi tutaona. Hebu wachache wasimame, chochote kile tu, na upate mahali pako hapo chini. Na ndipo tutaninii . . .

232 Lakini sasa kumbukeni, kila mtu aliye na kadi ya maombi, kama tu mtaendelea kuja, hatuwezi kuwaleta wote kwa wakati mmoja, bali tutawafikia upesi tu kama tuna . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mnaona?

233 Ni wangapi wanaojua ya kwamba nabii Danieli aliona ono naye alifadhaika kichwani mwake kwa siku nyingi? Hebu tuone ni wasomaji wangapi wa Biblia. Hakika. Vema, kama ono moja lilimdhoofisha Danieli, mnafikiri ninalistahimiliye siku baada ya siku, na usiku baada ya mwingine, na juma baada ya jingine, na mwaka nenda rudi? Kwa sababu Yesu alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya, na mengi kuliko haya.”

234 Sasa, toleo la King James linasema *kubwa zaidi*, bali wewe chukua tafsiri ya asili ya Kiaramu uone kama haisemi, “*Mengi kuliko* haya mtafanya.” Kwa maneno mengine, Yeye, Mungu alikuwa katika Mtu mmoja wakati huo, sasa Mungu yuko kote ulimwenguni, Yeye yuko ndani ya Kanisa Lake, kila mahali.

235 Sasa, tunajua ya kwamba utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa katika Yesu Kristo. Ni wangapi wanaamini hilo? Alikuwa ndiye utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Sasa, Roho yote iliyokuwa ndani Yake ingekuwa kama ziwa hili hapa nje, maji hayo yote, tuseme hayo yalikuwa ndiyo maji yote ulimwenguni. Lakini sasa, mimi na wewe tuna kijiko kimoja tu cha maji kutoka kwenye ziwa hilo, huyo ndiye Roho tuliye naye ndani yetu. Lakini kemikali zile zile zilizo katika kijiko hicho zimo katika hilo ziwa lote. Mnaona? Aina ile ile, asili ile ile, bali si kiasi hicho. Vema, hivyo ndivyo ilivyo hapa, si nyingi hivyo bali ni Roho yeye yule. Mnaamini hilo?

²³⁶ Sasa, naangalia tu kama ana watu wote kule chini. Sasa, kesho usiku...Ninataka kusema jambo fulani hapa wakati akiwaandaa. Ni wangapi wanaokumbuka wakati nilipokuja hudumani kwa mara ya kwanza, nilikuwa kwenye Pwani ya Magharibi, ningeunyosha mkono wangu namna *hiyo*, nao watu wanaweka mikono yao juu yake, na—nawe ungeweza kuliona kwenye mkono wako mwenyewe, watu waliokuwa na magonjwa, kijidudu cha aina yoyote? Ni wangapi wanaokumbuka hilo?

²³⁷ Sasa, ninyi watu wale wale mlionua mikono yenu, ni wangapi wanaokumbuka ya kwamba niliwaambia ya kwamba Malaika alikutana nami, kasema, “Kama utakuwa mwaminifu, uwafanye watu wakuamini, itakuwa kwamba utajua siri yenyewe ya moyo wao”? Ni wangapi wanaojua nilitabiri hilo? Mnaona? Kundi lilo hilo limeinua mikono yao. Vema. Sasa, ilitimia, Yeye alilifanya jinsi tu alivyosema. Sasa kuna jambo jipya linalotukia. Imerudi moja kwa moja mikononi mwa watu tena kuwaombea wagonjwa.

²³⁸ Hivi majuzi, ilikuwa ni msimu huu wa mwisho wa kupukutisha majani, moja ya mambo makuu sana yaliyotukia, huenda nikaingilia jambo hilo kesho usiku kabla sijaanza huduma hiyo ya kuwaombea wagonjwa, juu ya jambo ambalo lilikuwa la ajabu, ambapo sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu. Lakini ameniita tena niwaombee wagonjwa. Mkiupata huo ujumbe, upambanuzi. . .

²³⁹ Sasa, maono si kitu tu mnachowekeana mikono. Ni wangapi wanaojua ya kwamba karama na miito havina majuto? Hakika. Si kitu unachokishika. Unapozaliwa katika ulimwengu huu, unazaliwa na karama hizo. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakika, ndivyo.

²⁴⁰ Musa, asingeweza kujizuia kuwa Musa, sivyo? Yesu asingeweza kujizuia kuwa Yesu. Yohana Mbatizaji, miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, Isaya alimwona, nabii, akisema ya kwamba alikuwa ni sauti ya mtu aliaye nyikani. Mungu alimwambia Yeremia, “Kabla hujaumbika katika tumbo la mama yako, nalikujua, na kukutakasa, na kukuweka kuwa nabii wa mataifa.” Hiyo ni kweli. Mnaona? Ni kitu ambacho umezaliwa nacho.

²⁴¹ Sasa, maono kwangu...Jambo la kwanza ninaloweza kukumbuka, sikuwa na umri wa miaka miwili, nadhani, nilipoona ono langu la kwanza. Na kumekuwako na makumi ya maelfu yao, wala hakuna hata mojawapo ambalo limewahi kukosea, mnaona, kote ulimwenguni, kila mahali. Hilo ni thibitisho tu kwamba ninasema kweli, ni ushahidi wa Mungu kwamba ni kweli, Yesu yuaja.

²⁴² Sasa, msininii...Hatuninii...Sasa, tunajua ya kwamba Yesu anakuja katika siku ambayo wakati ulimwengu umelala usingizi na una uvuguvugu. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni

wangapi wanaojua ya kwamba huu ni Wakati wa Kanisa la Laodikia? Vuguvugu, watu tu, ninii tu, vema, wanaenda kanisani, na kusema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa,” hivyo karibu ndivyo, bali huo ndio wakati Yeye ajapo. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Amkeni. Mambo haya ni ya kufanya nini?

²⁴³ Sasa, sisemi ya kwamba Yeye atalifanya. Kumbukeni, siyadhibiti maono, maono hunidhibiti. Sasa, kuna wageni hapa ambao hawajawahi kuwa mkutanoni hapo kabla. Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, enyi watu wangu, kabla jambo lolote halijatukia, kama litatukia ama halitatukia, sijui, lakini kama likitukia kama tu Maandiko yasemavyo *hapa*, utamwamini Yeye, na kumwamini Yeye kwa ajili ya uponyaji wako? Inua mkono wako, useme, “Mungu,” namna hii, “ni—nitaamini.” Mungu awabariki.

²⁴⁴ Sasa, watu hawa katika...Ni wangapi walioko kwenye kusanyiko hili kwanza sasa, ambao hawana kadi ya maombi, nawe unataka Mungu akuponye? Inua mkono wako, huna kadi ya maombi, unataka Mungu akuponye. Vema. Kuwa tu na imani, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya, kuwa na imani, amini.

²⁴⁵ Hebu angalia hapa juu kwenye hili, useme, “Bwana, mtu huyo hanijui, bali jalia tu niwe na imani ya kutosha kugusa vazi Lako. Na halafu Wewe umeuke, umfanye mtu huyo, jalia Roho, najua isingeweza kuwa ni roho yake, maana yeye hanijui, lakini jalia Roho Wako Mtakatifu aingie humo ndani, kama ananiambia kweli, ageuke na kuniambia kama alivyomwambia yule mwanamke aliyeligusa vazi Lake.” Uone kitakachotukia. Jaribu tu, usijaribu, lifanye tu.

²⁴⁶ Sasa, wengi hapa...Ni wangapi kwenye mstari wa maombi ambao sijui chochote kuwahusu? Inueni mikono yenu. Ninyi watu mnaojua ya kwamba siwajui, inueni mikono yenu. Loo, kila mtu? Vema. Na huko nje, kwamba sikujui... .

²⁴⁷ Sasa, nina marafiki hapa, ninamwona Ndugu na Dada Palmer wameketi hapa kutoka Georgia, na halafu, huko nyuma mahali fulani kuna Ndugu Fred Sothmann, na Ndugu Norman, na, kutoka Arizona, najua wako hapa. Nao wako hapa mahali fulani mkutanoni, siwaoni, bali wako hapo ndani.

²⁴⁸ Na sasa, hawa wote ni...Na mwanamke huyu, hatufahamiani, sivyo, mama? Hatufahamiani? Hatufahamiani. Loo, ulikuwa hapa mkutanoni nilipokuwa hapa hapo awali? Lakini kwangu kukujua, nisingejua. Vema.

²⁴⁹ Ni wangapi hapa kamwe hawakuona wakati nilipoweka mkono wangu juu ya watu na kuona majibu kwenye huo mkono? Hebu tuone mkono wako. Vema. Tutawachukua tu kadhaa kama hao.

²⁵⁰ Njoo hapa kwa dakika moja. Sasa, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Mimi...Labda

tangu nilipokuwa hapa, nimeona watu milioni moja tangu wakati huo. Lakini sasa, kama . . . ninakutaka, chukua mkono wako . . . Sasa, kama ni kitu kama mateso, kama ugonjwa fulani wa kemikali ya damu, ama kiwete, ama yabisi kavu, ama chochote kile, ambacho si kijidudu. Mnaona? Itahitaji chembe hai, uhai mwingine.

²⁵¹ Ni wangapi wanaojua ya kwamba tumetokana na seli zazi, seli moja? Bila shaka. Tumetoka kwa baba zetu, himoglobini inatokana na jinsia ya kiume, ya kike ni yai. Lakini hiyo chembe ndogo . . . Na ninii yako— mwili wako umefanyizwa kwa chembe hai nyingi, bali ulikuja, asili yake, kutokana na chembe moja kutoka kwa baba yako. Hiyo ni kweli? Basi inafanya aina tofauti ya chembe hai karibu nayo. Hivyo ndivyo Kristo alivyokuwa Mungu, wakati Mungu alipojiingiza Mwenyewe katika Seli katika tumbo la uzazi la Mariamu, na akazaliwa, apate kutuokoa na dhambi, kwa kuvunjwa kwa Seli hiyo ya Damu ulimwengu unaokolewa, hapo.

²⁵² Sasa, kama ni mateso tu itabidi hayo yaonekane kwa njia nyingine. Lakini hebu tuone kama ni ugonjwa wa kijidudu. Kama ndio, mnaona, kungekuwa na chembechembe ya mauti juu yake ipate kumwua, nao ungetetemeka kama nina upako wa Roho Mtakatifu hapa pamoja nami.

²⁵³ Naam, bwana, ndivyo ulivyo, hakika. Ana ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Huu hapa, ana tumbo lenye vidonda. Unaona vizuri?

²⁵⁴ Ninataka kukuonyesha jambo fulani, nataka uangalie mkono wangu kwa dakika moja. Unaona jinsi mkono huo unavyoonekana umevimba, hivyo vitu vidogo vyeupe vikidunda juu yake hapo, vikipita juu yake? Unaona? Sasa weka mkono wako mwingine *hapa*, ili kwamba uone, geuza mkono *huu*. Sasa haupo, wa kawaida tu, mweupe, haujavimba, mkono tu wa mtu wa kawaida, sivyo?

²⁵⁵ Vema, sasa weka mkono wako mwingine papa hapa juu yake namna hiyo. Sasa, uangalie. Unaona tofauti yake, jinsi unavyovimba, unaona hivyo vitu vidogo vyeupe vikipita juu yake? Hivyo ndivyo nilivyokujua. Ni mtetemo, “*Whiu, whiu, whiu!*” Ni kijidudu, unaona. Sasa, sasa, angalieni si mahali tu ninaposhikilia mkono wangu, mnaona popote vilipo.

²⁵⁶ Sasa, ni nani aliyesema hawakuwa wamewahi kuona jambo hilo? Ilikuwa ni wewe, Ndugu Borders? Ulikuwa umeliona? Mtu fulani alikuwa ameniambia ya kwamba hawajawahi kuliona na walitaka kuona. Basi, sawa, njoo hapa Ndugu Folst. Ni wangapi wanaomjua huyu muungwana hapa? Inua mkono wako. Nadhani ninyi nyote mnamjua, anatoka kwenye mji huu hapa.

²⁵⁷ Nataka uangalie hapa, Ndugu Folst. Hivi ndivyo ninavyojua hilo. Sasa, angalia hapa. Ati hujawahi—hujawahi kuona huduma hii ikifanya kazi? Vema. Sasa, hivi majuzi usiku. . . Siwezi kuvaa

saa ya mkononi *hapa*. Nilikuwa na Longines ya dola mia mbili niliyopewa kutoka kwa Lichen hapa chini, ikaanguka kwenye ninii yangu. . . mimbarani. Halafu hivi majuzi usiku nilikuwa na Vulcain Cricket ya dola mia tatu, niliyopewa kutoka huko. Na huko juu mkutanoni hivi majuzi usiku. . . Wangapi walikuwa kule hivi majuzi alasiri? Nami. . . Hapa juu kwenye Maporomoko ya Klamath, ndipo Vulcain Cricket ya dola mia tatu ikaanguka kutoka mkononi mwangu. Mikono ikatoka, shina likatoka, ikatengana nayo, kwa kuushika tu mkono wa mtu namna hiyo. Kwa nini? Siwezi kuwaambia. Sijui. Lakini huwezi kushikilia saa kwenye huo.

258 Sasa angalieni, ninawatakeni muuangalie mkono wangu. Mnaona? Mnaona? Chukua mkono wake, mkono wa kulia tu, hebu tuone, ama ninamaanisha, mkono wake wa kushoto, ni mamoja tu. Sasa angalia ninapougusa mkono huu *hapa*. Hiki hapa kinakuja. Mnauona ukivimba? Mnaona vitu hivyo vidogo vyeupe vikirukaruka juu yake?

259 Sasa, mnaona, sasa, ni—ni kitu gani kilichochukua mkono wake wa kuume? Hivyo ndivyo alivyoniambia, “Mkono wao wa kuume kwa mkono wako wa kushoto.” Huyu ni yeye na mkono wake wa kuume akiniahidia imani yake, sawa, nami ninamshika mkono wa kushoto huku mkono wangu mwingine ukiwa kwa Mungu. Mnaona? Sasa, haitafanya kazi kwa njia nyingine yoyote.

260 Sasa, unaweza kuliona. Angalia hapa, ndugu, angalia hapa, unaona, nauweka mkono wangu juu ya mkono wake. Unaona? Chini mahali ilipo, ni vile vile tu. Unaona? Sasa chukua tu mkono *huu hapa*, sasa angalieni kinachotukia mara tu ninapoushika mkono wake. Hicho hapa. Mnaona, jinsi unavyowaka moto? Ni kama tu kuchukua *kiasi hicho*, kama mkondo wa umeme mkononi mwako, hivyo vitu vidogo vyeupe, mnaona? Sasa tulieni tu kabisa. Sasa, inasema kile kilicho. Unaona?

261 Sasa, huko ni kuutambua. Sasa, utaondoka? Sasa, dada, u—unaamini sasa? Unaniamini kweli? Vema. Sasa nataka kila mtu awe na kicho, nami ninawatakeni mwinamishe kichwa chenu. Sasa ninataka hawa—hawa watu wawili *hapa* wasimame hapa mahali nilipo. Sasa, nawatakeni muone, ndugu, mnaona, ili kwamba muone si mahali pake, mahali ninapoushika mkono wangu, mnaona, panaposababisha vitu vyeupe vitiririke juu yake na kuufanya ugeuke hivyo. Mnaona?

262 Sasa, unaliona dhahiri, sivyo, dada? Mnaweza kuviona vyote papo hapo, ninapozungumzia? Mnaona jinsi unavyovimba na kuwa mweupe, mnaona, unapata vitu halisi, vidogo vyeupe? Basi unaona, na kukuthibitishia ya kwamba jambo fulani linaendelea, inajua una shida gani. Hiyo ni kweli moja kwa moja. Unaona? Sasa, unaona jambo fulani. Sasa, angalia—angalia

hapa, naweka mkono wangu juu ya wangu. Unaona? Unaona? Huyu hapo anakuja. Unaona? Mara anaponigusa hapo inaanza.

²⁶³ Sasa, nitaninii...Ninajua nyote wawili ni Wakristo. Sasa kumbukeni, mambo haya yatakapotokea...Nitajaribu kumkemea. Mnaona? Na kama akitoka...Sasa, Biblia ilisema wakati wao...wakati jamaa mmoja wakati mmoja alipojaribu kumtoa pepo, nanyi mnajua kilichotukia. Kwa hiyo sasa, kama akitoka, atakuwa huru, atakuwa akifanya ninii yoyote... atamwendea mtu yeyote, na ni ugonjwa wa tumbo.

²⁶⁴ Sasa, ninawatakeni katika kusanyiko ku—kuinamisha kichwa chenu. Na hawa hapa mashahidi watatu wamesimama hapa. Sasa, siwataki. Njoo huku juu. Unaona? Mnaona, wakati mwingine humwingia asiyeamini. Mnaona? Ndipo bakshishi inanjia kutoka mkutanoni. Unaona? Lakini na—nawajua ninyi nyote, nimekuja kwenu. Mnaona? Vema. Sasa angalieni, nitaunyosha tu mkono wangu papa hapa. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Sasa, angalieni, na uangalie, pia, mama, mkono.

²⁶⁵ Sasa tutaomba, kila mtu awe katika maombi pamoja nami. Sasa, wataangalia. Sasa, sininii...Yesu alisema, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Vema, sasa, hilo likikoma sasa hivi, kamwe sitasogeza mkono wangu, kama vikisimama na kugeuka kama mkono huo, vema, usipofanya hivyo basi siwezi kusaidia. Sasa na tuombe.

²⁶⁶ Baba wa Mbinguni, ili kwamba Jina Lako lipate kutukuzwa, hatuombi miujiza, bali Bwana, huduma hizi zinazidi kukua, Yesu yuaja hivi karibuni, ninaomba ya kwamba utamrehemu dada yetu na utamponya. Huyu hapa amezeeka, na hawezi kula, Bwana, hili ni jambo baya sana, na mara ya mwisho hapa, Wewe ulimponya mwanamke aliyekuwa akifa, na, kwa jambo lile lile, ila baya tu zaidi. Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utambariki na kumponya, katika Jina la Yesu.

²⁶⁷ Sasa, ni...Sasa, sijafungua macho yangu bado, lakini, ndugu, niambie, angali pale kama tu alivyokuwa. Hiyo ni kweli? Hajaondoka, hajaondoka. Sasa, itatubidi kuja na mamlaka ya kumtupa nje. Sasa, hatuombi Baba, nyote mnaelewa, siombi Baba atufanyie mwujiza, maana ni kizazi kiovu na cha zinaa kinachotafuta miujiza, lakini ili upate kujua ya kwamba Yeye angali ni Mponyaji.

²⁶⁸ Sasa, hebu tuangalie tena sasa. Hebu na tuwe ninii halisi—halisi...Mko katika maombi kila mmoja wenu, mnaona, mumefunikwa na Damu.

²⁶⁹ Sasa, Baba wa Mbinguni, watu hawa wanatazama, mwanamke huyu anaangalia kama shahidi. Ninamwombea mwanamke huyu, hapana shaka ameombewa mara nyingi. Lakini, Baba Mungu, kama kuna jambo lolote maishani mwake ambalo si sahihi, basi Baba, Wewe liondoe, unaona.

²⁷⁰ Sasa, kama kuna kitu chochote kingehifadhi, ama, kingehifihadhi roho hii, kama ungeifanya iondoke, kama ingerudi. maana tunajua itaenda na kutembea mahali pakavu kisha irudi tena, ikiweza. Lakini kama hakika anaona ukweli huu wote na ushahidi, ataamini kwa moyo wake wote. Ninakuomba uturehemu.

²⁷¹ Wakati watu hawa wakiangalia, kuna macho ya wanaume wawili na mwanamke mmoja yanayoangalia moja kwa moja mkononi mwangu, huku macho yangu yamefumbwa:

²⁷² Shetani, ewe pepo mchafu ambaye angemchukua maskini mwanamke mkongwe namna hii na kumtendea mabaya, mbona, wewe ni mwovu, huna mamlaka ya kumshikilia, yeye ni Mkristo, nami ninakuja, katika Jina la Yesu Kristo, dhidi yako. Ninakuja nikishuhudia karama ya uponyaji wa Kiungu kuwaombea wagonjwa, ambayo Malaika alinihudumia, miaka kumi na minne iliyopita, na kuniambia juu ya karama zingine zinazokuja. Unajua jambo hili. Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, toka ndani ya mwanamke huyu, mwache, toka ndani yake, hata isimsumbue tena, katika Jina la Yesu Kristo!

²⁷³ Sasa, ndugu, sijawahi kuusogeza mkono wangu, lakini ameondoka sasa, sivyo? Ameondoka kabla sijafungua macho yangu? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.]

Vema, unaweza kuinua kichwa chako.

²⁷⁴ Sasa, sasa angalia *hapa*, dada mpendwa, weka mkono *huu hapa*. Mnaona jinsi unavyoonekana? Sasa, mnaona jinsi unavyoonekana? Sawasawa tu na... Mnaona? Mnaona, sawa kabisa. Sasa, jambo fulani lilitukia, sivyo? Ugonjwa wako wa tumbo umekwisha, uko huru. Nenda nyumbani ukashangilie, uwe na furaha, na umshukuru Bwana mpendwa kwa uponyaji wako. Vema. Mungu akubariki, dada. Vema.

Unaamini kwa moyo wako wote?

Sasa hebu tuone kuhusu huyu dada hapa. Hivi hatufahamiani? Hatufahamiani. Vema.

²⁷⁵ Sasa, kila mtu awe na kicho. Tutachukua tu muda wetu ili kwamba mwe na imani, wakati wenu wa kuombewa unapowadia. Kama watu hawa katika Biblia usiku wa leo, walikuwa na imani. Yesu alisema, "Kama nikizitenda kazi za Mungu, basi ziaminini hizo kazi." Mnaona?

²⁷⁶ Sasa, hebu niushike mkono wako kwa dakika moja tu. Sasa, una shida kidogo ya akina mama, lakini hiyo kweli siyo iliyokuleta. Unaona? Hebu kidogo. Sasa, hii itabidi ije kwa ono. Naam, ni kisukari, ugonjwa wa sukari. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Kisingeonekana *hapa*. Ana shida ndogo ya kike, lakini haitoshi kwa hilo, kwa sababu asingetambua hiyo sana, bali ni kisukari.

277 Sasa unaona, hapo kisingeonyesha kamwe, maana hiyo ni sehemu ya kemikali, kisukari, mnaona, ni—ni kemikali, ni sukari kwenye damu.

278 Sasa, kama Bwana Yesu anaweza kusimama hapa na kuniambia una shida gani, kama tu vile Yeye angeweza kumwambia yule mwanamke kisimani, ama, kumwonyesha, ni Yesu yeye yule? Unaamini.

Sasa na tuombe.

279 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja katika Jina la Bwana Yesu na kuomba kwamba jambo hili ovu limwache dada yetu. Jalia aende na awe huru na huu, na apate afya. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

280 Sasa, “Maombi ya imani yatamwoko mgonjwa yule, Mungu atamwinua.” Nenda sasa. Mungu awe pamoja nawe. [Dada mmoja anasema, “Hiyo itaponya macho yangu, pia?”—Mh.] Wasemaje? [“Hiyo itayaponya macho yangu, pia?”] Loo, hakika, hilo ndilo linalosababisha jambo hilo, unaona. Hiyo ni kweli. Na Mungu akubariki, dada. Vema.

281 Njoo, msichana. Hivi hatufahamiani? Vema. Sasa, hebu tuone mkono wako, mkono *huu* hapa upande *huu*. Uko sawa. Um-hum. Sasa, inahitaji ono kwa ajili yake, unaona.

282 Sasa vinginevyo, huduma yangu ya mwanzoni, ni wangapi wanaojua katika huduma yangu ya mwanzoni kamwe nisingejua alikuwa na shida gani mwanamke huyo, mnaona, maana hakuna mtetemo.

283 Sasa hebu tuone tu dakika moja. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Au una—unaamini yale ambayo nimefundisha usiku wa leo kuwa ni kweli? Mimi ni mtumishi Wake. Naam, ugonjwa wa moyo. Sasa, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa moyo? Unaamini hilo, kwamba Yeye atauponya huo moyo. Wewe ni msichana mdogo tu, sasa, mwenye wasiwasi. Sasa, kama Yeye atauponya, utampa sifa kwa ajili yake?

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

284 Baba yetu wa Mbinguni, tunaomba sasa ya kwamba katika Jina la Yesu Kristo kwamba nguvu za Mungu zitakuja juu ya msichana huyu, na jalia aponywe ninapoweka mikono yangu juu yake. Watu... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... wanaajua, Bwana... [Sehemu tupu kwenye kanda.] Hiyo ni...?... [Sehemu tupu kwenye kanda.]

285 ...Nadhani ndivyo, mara ya kwanza. Vema. Sasa, huyu hapa mwanaume ambaye sijawahi kumwona. Huyu ni mwanaume. Sasa, kulikuwa na mtu aliyemjia Bwana Yesu jina lake Simoni Petro. Mnakumbuka hadithi niliyohubiri juu yake usiku wa leo? Vema. Sasa, ndipo Yesu akanena, akamwangelia ameketi pale kwenye kisiki hicho. Mlinisikia nilipohubiri usiku wa leo?

Akasema, “Jina lako ni Simoni, mwana wa Yona.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁸⁶ Sasa, kwamba Yesu angali anaishi? Je, kusanyiko linaamini hilo? Vema. Kama huyo Yesu yu hai, nami ni shahidi Wake wa kweli, basi na—najitoa mwenyewe kwa karama . . .

Sasa, kama ungesema, “Niponye.”

²⁸⁷ Mbona, Yeye angesema, “Tayari nimefanya hivyo.” Ni wangapi wanaoamini ya kwamba tayari amefanya hivyo huko nyuma Kalvari wakati alipokufa kwa ajili yako? “Alijeruhiwa kwa . . .” Hakika.

²⁸⁸ Lakini sasa, kuwafanya mjue ya kwamba Yeye yu hai hapa kuthibitisha Neno Lake, huenda akakwambia kitu kama alivyomwambia Petro, ama baadhi yao, angekwambia jambo fulani kukihusu. Kwamba . . . Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini . . .

²⁸⁹ Sasa, hebu tuone kama Yeye atalifanya, niamini tu kama mtumishi wa Mungu. Vema. Anasema anajua atafanya hivyo. Hakika, ni pua yako. Hiyo ni kweli. Hiyo ni pua yako. Sasa, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

²⁹⁰ Sasa, mtu fulani anasema . . . Sasa, nilishika hilo. Usiwazie hilo sasa. Usifanye hivyo, hilo linanizuia. Unaona? Kamwe sikubahatisha hilo, huko hakukuwa ni kubahatisha. Unaona? Hapana.

²⁹¹ Hebu kidogo. Anaonekana kuwa mtu mzuri sana. Simama kimya kwa dakika moja tu, simama tu kimya, bwana. Naam, bwana. Ni pua yake, ana kitu kidogo ambacho huingia ndani yake, amefanyiwa upasuaji kwa ajili yake. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Akafanyiwa upasuaji, na i—inaonekana kana kwamba kitu hicho kinarudi tena, ni namna fulani ya, kitu kama, vivimbe ama jipu, kama, puani. Hiyo ni kweli. Inaonekana kana kwamba haifanyi vizuri. Hiyo ni kweli, siyo? Huko si kubahatisha.

²⁹² Hebu nikwambie jambo fulani. Ninamwona mwanamke akitokea, ni mkeo. Yuko nyumbani. Unaamini hilo . . .? Anaomba, ni mgonjwa. Unaamini Mungu anaweza kunifunulia shida yake ni nini? Ana ugonjwa wa moyo na yabisi kavu, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bw. Boggs, nenda nyumbani na uwe mzima, Yesu Kristo anakuponya kama ukiamini. Amini . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁹³ . . . hatufahamiani, dada? Umekuwa katika . . . Lakini ninamaanisha huko nje katika . . . Sininii . . . mimi . . . Hujawahi kukutana nami, binafsi, sijawahi kukutana nawe. Lakini ikiwa Bwana Yesu, huyu hapa mwanamke, ikiwa Bwana Yesu anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu, kama mwanamume na mwanamke, kama vile Yeye na yule mwanamke kisimani, huyo alikuwa ni mwanamume pale, sasa, kama yule mwanamke

kisimani, kama anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu wewe ambalo unajua nami sijui, kilichokuleta hapa, huenda ikawa ni kwa ajili ya mtu mwingine, huenda ikawa ni shida ya kifedha, huenda ikawa ni shida ya kinyumbani, huenda ikawa wewe ni mgonjwa, sijui, lakini kama Yeye ataniambia, utamwamini kwa moyo wako wote?

Je, kila mwanamke hapa ndani ataamini kwa moyo wao wote? Vema. Bwana na atujalie.

Huyo mama aliyeketi papo hapo akiwa na mishipa iliyovimba, unaamini Yesu Kristo atakuponya? Ulikuwa unaomba, sivyo? Vema.

Aligusa nini? Alimgusa Kuhani Mkuu, Yesu Kristo.

²⁹⁴ Nilimwona mwanamke amesimama hapa mbele yangu akiwa na kitu fulani, kama karibu damu ikitiririka kutoka kwenye mishipa, haikuwa ni mwanamke huyu, kidogo alikuwa mzito kuliko mwanamke huyu. Nikaangalia, nikawaza, “Hapo ni wapi?” Ndipo nikaangalia, na nikaona ile Nururu. Ni wangapi wameiona ile picha ya ile Nururu? Vema. Alikuwa amesimama juu ya yule mwanamke pale, akizungukazunguka, nikamwona, hiyo ilikuwa ndiyo shida yake. Mnaona? Naam, bwana. “Kama utaamini!”

²⁹⁵ Uliyeketi hapo ukiwa na lesa yako mkononi mwako ukiwa na kikohozi kiletwacho na vumbi, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, pia? Vema. Uligusa nini? Sasa, huo si ugonjwa. Ninakuona ukilemewa na mizigo, umeshikilia ninii yako... , ukipiga chafya, ukiendelea, unaona. Amini tu, utapona, pia.

Unamwamini Yeye kwa moyo wako wote?

Una uvimbe mgongoni. Unaamini ya kwamba Mungu angeweza kukuponya? Hiyo ni kweli? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuuondoa? Vema.

Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utambariki mwanamke huyu, na kumpa afya, ninapambariki, katika Jina la Yesu. Amina.

Nenda, Bwana na akubariki.

Roho angali ndani ya jengo.

²⁹⁶ Uliyeketi hapo ukiwa na bawasiri, unafikiri ya kwamba Mungu atakuponya? Ulikuwa unalia, ukiomba, “Bwana, jalia aguse... Na aniite.” Kama hiyo ni kweli pungu mkono wako huku na huku namna *hii*, wewe uliyeketi hapo. Unaona? Ningejuaje kile ulichokuwa ukiombea?

²⁹⁷ Hivi hamfahamu ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu? Aligusa nini? Kuhani Mkuu yule yule ambaye maskini mwanamke yule alimgusa aliyekuwa aki—akitokwa na damu. Simjui huyo mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu. Vema, ameketi yadi ishirini kutoka kwangu, naye

akamgusa, Akageuka, akasema, “Angalia *pale*.” Niliiona Nuru Yake kule, nami nikaona kile alichokuwa anaogua. Na hilo hapo, mwanamke huyo atapona, atakuwa mzima. “Kama tu utaamini!”

²⁹⁸ Sasa yeyote kati yenu, ninaipa imani yako changamoto, katika Jina la Kristo, mahali popote, kuliadini. Vema.

Mimi na wewe hatufahamiani? Nadhani hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana.

Sasa kwa uchaji tu, kidogo tu.

Kama Bwana Yesu atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo unajua kwamba silijui, itakufanya uadini kwa kile ulicho...?

Itafanya wasikilizaji hivyo, pia?

²⁹⁹ Ni yabisi kavu, una yabisi kavu. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ili iweze kukuondolea huko kubahatisha, unaona, una jambo fulani niani mwako ambalo linakusumbua sana, vibaya sana. Sasa, kama Bwana atanifunulia hilo, utaniadini kwa moyo wako wote? Ni mume wako. Hayupo hapa, hata hayuko katika mji huu, yuko katika mji mwingine unaoitwa Ukiah ama kitu kama hicho. Ana ugonjwa ambao unaua, unaitwa Parkinson, ugonjwa wa Parkinson. Hiyo ni kweli.

³⁰⁰ Una mtu fulani pamoja nawe usiku wa leo, pia, ambaye unataka aombewe, ni mjukuu mdogo, ana shida ya macho. Jina lako ni Bibi Zigler. Vema. Nenda na uadini kwa moyo wako wote, na unaweza kupata kile unachoomba.

³⁰¹ “Kama unaweza kuadini!” Una—unaadini sasa kwa moyo wako wote?

³⁰² Sasa angalia, upate kujua, ninii tu, nitamruhusu mama huyu, weka tu mkono wako juu ya wangu, mama. Wewe... Kama Bwana atanifunulia shida yako ni nini, unaniadini mimi? Basi ugonjwa wako wa moyo umekwisha. Nenda, amini, upate afya. Mwamini Mungu, amini kwa moyo wako wote.

³⁰³ Angalia hili: Unaadini yabisi kavu yako itakuacha? Vema, sawa nenda zako, useme, “Asante mpendwa Yesu.” Naam, mama. Amini tu kwa moyo wako wote.

³⁰⁴ Vipi kama sikukwambia chochote, nikuwekee tu mikono, ungefikiri ungepona? Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukawe mzima. Amina. Amini sasa.

Una wasiwasi. Hivi huadini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya, akupe afya? Nenda tu ukiamini, Yeye amekuponya, atakuponya.

Unaadini huko nyuma uliponywa ulipokuwa ukipanda vipandio? Endelea tu kusonga mbele, ukisema, “Asante Bwana,” na upate afya.

305 Ni wangapi huko nje unayeamini kwa moyo wako wote? Je, una hakika kwamba Yesu angali anaishi? Sasa, una hakika? Je, *unajua*? Hii hapa Biblia yangu juu ya moyo wangu, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo? Nililisoma kutoka katika Biblia hapa ya kwamba Yeye hufanya hivyo, Yeye aliliahidi, alilifanya jana, Yeye analifanya leo. Sasa, kuhusu uponyaji, uponyaji wako tayari umenunuliwa katika Damu, unaamini hilo. “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*,” wakati uliopita. Lakini Yeye anathibitisha Neno Lake kwa kuwa hapa kukujulisha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nyote mnaamini hilo kwa moyo wenu wote?

306 Sasa, ni waaminio wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu. Sasa, kama Mungu akitimiza Neno moja, Yeye hutimiza Maneno yote. Hiyo ni kweli? Sasa, je, Yeye alisema hivi: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya”? Ni wangapi wanaoamini hilo? Vema, basi ninyi nyote ni waaminio. Sasa wekeaneni mikono, wekeaneni tu mikono, hiyo ni kweli. Haya basi. [Dada mmoja anapiga mayowe katika Roho—Mh.] Hivyo ndivyo linavyoenda, hilo hutukia. Hivi hamjui Yeye yupo hapa? Wekeaneni mikono, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

307 Ishara hizi zitafuatana na nani? Mwaminio, mwaminio. Sasa wewe mwombee mtu uliyemwekea mikono. Usijiombee mwenyewe, mwombee mtu uliyemwekea mikono.

308 Baba yetu wa Mbinguni, tunawaleta wasikilizaji hawa Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, ambaye juu yake Roho Mtakatifu yuko hapa sasa, akitoa ushahidi, akiumimina Uwepo Wake, akifanya kila mtu ajue ya kwamba Yeye yupo, kwamba hajafa, kwamba Yu hai milele, Naye anaweza kuwasaidia wale wanaomjia, kuwapa uponyaji. Kusanyiko linajua ya kwamba kuna Kiumbe cha kimbinguni miongoni mwao usiku wa leo, yule Roho Mtakatifu anayefunua siri za moyo, ya kwamba Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia. Waaminio hawa wamewekeana mikono, wanaamini.

309 Baba, Mungu, umeshuhudia ya kwamba Wewe upo hapa, nisikie, Bwana. Ninatoa kila roho ya kutokuamini, acha liondoke kwenye jengo hili, na liwaondoke watu, kitu pekee kinachoweza kuwazuia kuponywa.

310 Shetani, umeshindwa vita, umefichuliwa, umefichuliwa hapa usiku wa leo. Ninakuapisha, katika Jina la Yesu Mwana wa Mungu, toka kwenye kusanyiko hili, toka kwa watu, huku wamewekeana mikono! Ninawapa uponyaji wao, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

311 Wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. Endeleeeni kuamini, mkiamini, na wakati nguvu za Mungu zinapokuja juu

yako, basi simama kwa miguu yako na umpe Mungu sifa.

³¹² Vema, Ndugu Folst. 

60-0720 Ni Mimi
Lake County Fairgrounds
Lakeport, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org